# Nipashe

Ijumaa Desemba 20 , 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580106

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure




## Muuguzi atuhumiwa kumbaka mjamzito akisubiri kujifungua

UKURASA 4

# Mbowe atangaza dawa wasaliti wa Chadema

**SALAMU** zake baada ushindi; Lissu asomba 98%...*Endelea ukurasa wa 2*




Kijana muuza kofia za Father Krismasi akizitembeza kwa wenye magari Barabara ya Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaan jana, yakiwa ni maandalizi ya Sikukuu ya Krismas inayotarajiwa kusherehekewa Jumatano ijayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**MBARONI KWA TUHUMA KUJIITA BOSI TAKUKURU**
MKAZI wa Mbagala wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, Hussein Hassani (43)...

**UKURASA WA 3**

**WADHAMINI WA TUNDU LISSU WAPEWA KIBANO KIKALI**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewasisitiza wadhamini...

**UKURASA WA 7**

**MAKOSA YA JINAI YAPUNGUA KWA 2%**
JESHI la Polisi nchini limesema kuwa makosa makubwa ya jinai yamepungua kwa asilimia 2.0...


## TCRA YAFUNGUKA KUZIMWA LAINI SIMU

UKURASA 4

# Aliyetimuliwa UDSM awatuliza wanafunzi

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** USAJILI YANGA KAMA WA DIRISHA KUBWA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Mbaroni kwa tuhuma kujiita bosi Takukuru

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mbagala wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, Hussein Hassani (43), ametiwa mbaroni na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa tuhuma za kughushi kitambulisho, kutapeli kwa kujiingizia kipato kwa kujifanya ofisa wa taasisi hiyo.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, aliyasema hayo jana jijini wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo.

Alidai Hassani alighushi kitambulisho chenye utambulisho wa taasisi hiyo kilicho na namba PCCB 1565 na jina Hussein M. Mhando kilicho na cheo 'Principal Investigation'.

"Taarifa ilipotufikia Takukuru Desemba 12, mwaka huu, tulimwekea mtego maeneo ya Pachoto, Mwananyamala. Kwa bahati mbaya, alikimbia baada ya kuwaona watu asiowafahamu, alikimbia kwa kutumia gari namba T618 DMS," alidai. Myava alidai walifanikiwa kumkamata baada ya kumwekea mtego wa pili Desemba 16, mwaka huu, baada ya maofisa wa taasisi hiyo kuliona gari lenye namba hizo na kulikamata na baadaye yeye mwenyewe kujisalimisha baada ya kuona gari lake linashikiliwa bila kujua tuhuma zinazohusishwa na gari hilo.

"Uchunguzi utakapokamilika, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya mtuhumiwa kwa mujibu wa sheria. Takukuru inatoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa kuhusu matukio hayo kupitia namba 113 bure," alisema.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akimuelezea jambo Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alipokutana naye jana katika ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPGAPICHA WETU**

# Mbowe atangaza dawa wasaliti wa Chadema

**Na Waandishi Wetu**

SHANGWE na nderemo zililipuka ukumbini mara tu baada ya Freeman Mbowe kutangazwa kurejea kwenye uenyekiti wake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) jana alfajiri.

Ni tukio lililokuwa sehemu ya kukamilisha mchakato mrefu wa uchaguzi, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akiwa miongoni mwa mashuhuda waliokesha kulisimamia.

Hoihoi na nderemo ziliutawala Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam, kidokezo kikuu kikimpamba Mbowe kwa kauli 'mwamba tuvushe' iliyoendana na kumnyanyua kwa furaha.

Mwenyekiti mkongwe ndani ya Chadema, alitumia fursa hiyo kutangaza rasmi viti dhidi ya alichokieleza kuwa ni usaliti ndani ya chama na wakati huohuo kumpelekea salamu Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, akidai asipende kuwatia hofu wanasiasa.

"Ndani ya chama chetu wamekuwapo wasaliti wa njia mbalimbali, wa staili mbalimbali na hawakuisha juzi wala jana na hawataisha leo wala kesho, wajibu wetu kama wana Chadema ni kukipenda chama chetu kwa wivu uliokithiri.

"Lakini, pale yeyote atakapojaribu kwa

INAENDELEA UK. 8


**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na First National BankTanzania Limited (FNB Bank) Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) yake kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndugu: **FELISTER RICHARD JACHI** | Nyumba ya makazi yenye hati na.64966 kiwanja na.410 Kitalu"GG" eneo la Baraa jiji la Arusha iliyopo kwa jina la FELISTER RICHARD JACHI | 10/01/2020 |

MASHARTI YA MNADA

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE: +255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
First National Bank Tanzania (T)Ltd.
FNB House,
Ohio Street,
P.O.BOX 72290
DAR ES SALAAM
Tel: + 255 768 989 000
Email: info@fnb.co.tz

115562402


# Aliyetimuliwa UDSM awatuliza wanafunzi

**Na Salome Kitomari**

KATIBU wa Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP), Joseph Malekela, amewatuliza wanafunzi wenzake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kutofanya vurugu au kuandamana kwa kuwa serikali imeshughulikia malalamiko yao ya fedha za mikopo kwa kiwango kikubwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Malekela ambaye ni miongoni mwa wanafunzi watano waliosimamishwa kwa muda usiojulikana na uongozi wa UDSM, alisema yaliyotokea dhidi yao ni wajibu wa kiuongozi na wanabeba jambo hilo.

Aliwataka wanafunzi kuendelea na masomo yao huku akieleza kuwa hawakuwa na lengo la kufanya vurugu, bali kuiamsha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB).

"Naombeni niwaweke wazi kwamba, hakuna aliyekuwa na nia mbaya ya kuleta vurugu. Amani ni kitu cha msingi katika nchi yetu. Lakini kwa kiongozi, maslahi ya anayewaongoza, ni jambo muhimu zaidi kuliko maslahi yake. Kiongozi hawezi kulala wakati watu wake wanataabika," alisema.

Kiongozi huyo wa wanafunzi pia aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter jana kuwa: "Kwa kuwa suala la msingi lilikuwa maslahi ya wanafunzi, na tayari serikali kupitia Wizara ya Elimu wameshachukua hatua za haraka kutatua, huku viongozi tumeshabeba huu mzigo kwa kuhatarisha masomo yetu, hakuna umuhimu wa wanafunzi kuleta vurugu, tuachieni sisi na mtulie,

"Ninaamini CKD italitazama hili suala kwa kina. 'All ni all' (yote kwa yote), lipo jambo la kujifunza katika haya yote na kwa yeyote. Watu ambao wana nafasi kama yangu msiogope. Watumikieni watu, uongozi siyo jambo 'simple' (rahisi). Simamieni haki na muhimu zaidi lindeni amani.

"Kimsingi, uongozi siyo kazi rahisi. Nilikubali kuwa kiongozi, tena katika nafasi ngumu kuliko zote, na nyie ni mashahidi, mimi pamoja na wenzangu tumejitahidi sana kusimama kwa ajili yenu na kupambania maslahi yenu. Na kubwa zaidi tumeyavaa maumivu ya maslahi yenu."

Malakela pia alihojiwa na vyombo vya habari vya kimataifa juzi jioni na kueleza kuwa kabla ya kutoa siku tatu kwa HESLB, walikuwa wameshafanya mazungumzo na uongozi wa bodi hiyo tangu vyuo vilipofunguliwa Novemba 4, mwaka huu na hakukua na mafanikio.

"Serikali ya wanafunzi ilibaini baadhi ya wanafunzi wana madai na kutoa uamuzi wake ndani ya muda fulani mambo yawe yametekelezwa, lengo si kuleta vurugu au kuandamana kwa sababu kulikuwa na mazungumzo.

"Pamoja na hatua za kusimamisha baadhi ya wanafunzi, yale madai ya msingi yametekelezwa na serikali imeahidi kutekeleza baadhi ndani ya wiki hii. Hizi hatua pamoja na kwamba zimekuja katika hali isiyo nzuri, wanafunzi

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Agnes Kuhenga na kiongozi wa timu ya madaktari kutoka China wanaofanya kazi nchini, Dk. Quin Chengwei, wakiweka saini makabidhiano ya dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 15 zilizotolewa na China kwa ajili ya wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kuchangia gharama za matibabu wanaotibiwa katika Taasisi hiyo jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: ANNA NKINDA**

# TCRA yafunguka kuzimwa laini za simu Desemba 31

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imefunguka kuhusu kufungwa kwa laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa mfumo wa vidole Desemba 31, mwaka huu.

Mamlaka hiyo imesema kwamba hakuna laini ya simu itakayofungwa kabla ya tarehe hiyo. Aidha, imesema wananchi wanatakiwa kwenda kusajili laini zao kwa kutumia vitambulisho vya uraia, na kuthibitisha usajili huo kabla ya muda uliowekwa kwa kuwa hakutakuwa na mabadiliko ya kuzifunga.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kaimu Meneja Mawasiliano wa TCRA, Semu Mwakanjala, alisema hadi sasa laini za simu milioni 20 zimesajiliwa.

"Hakuna mabadiliko yaliyotolewa ikifika Disemba 31, mwaka huu, laini zote ambazo hazijasajiliwa kwa namba ya Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) na kuthibitisha kwenye mifumo zitafungwa, tunawakata wananchi wasajili haraka," alisema.

Aidha, alisema hakuna mtoa huduma atakayeruhusiwa kufunga au kukatisha mawasiliano ya mtumiaji yeyote kabla ya muda uliopangwa.

Jana kwenye baadhi ya makundi songezi (WhatsApp) baadhi ya watumiaji wa laini za simu walilalamika kukosa mawasiliano kwenye baadhi ya laini kwa kile kilichoelezwa kuwa zimezimwa kwa kuwa hawajasajili.

Mei mwaka jana, serikali ilitangaza ulazima wa usajili wa laini za simu, na kwamba ifikapo mwishoni mwa mwaka huu zitafungwa.

# Wadhamini wabanwa kumpeleka Lissu makamani vinginevyo...

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewasisitiza wadhamini wa Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki (Chadema), Tundu Lissu, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi wampeleke mshtakiwa huyo vinginevyo fungu lao la dhamana litafyekwa.

Kadhalika, mahakama hiyo imewaagiza wadhamini hao, Ibrahim Ahmed na Robart Katula kuhakikisha mshtakiwa anakwenda kwa ajili ya kuendelea kusikiliza kesi hiyo ushahidi wa Jamhuri.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya kumhoji mdhamini kuhusu amri yake ya awali iliyowataka kumpeleka Lissu mahakamani.

Alisema wadhamini waongeze jitihada wampeleke mshtakiwa kabla sheria haijachukua mkondo wake dhidi ya wadhamini hao.

Awali, Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, alidai kuwa upande wa Jamhuri unashindwa kuita mashahidi kwa sababu mshtakiwa wanne hayupo mahakamani.

Alidai kuwa wanashindwa kuelewa mshtakiwa yuko wapi, bado mgonjwa au anafanya nini kinachomkwamisha kufika mahakamani.

Ahmed alidai kuwa Lissu amepona, lakini ana shaka kurudi nchini.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 20, mwakani na wadhamini wampeleke mshtakiwa huyo.

Mbali na Lissu, washtakiwa wengine ni, WA Hariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na

INAENDELEA UK. 8

# Ofisi ya Rais yashtukia matumizi ya bil. 100.5/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamuhanga, amesema Ofisi ya Rais inaendelea kufanya tathmini kwa hospitali zote 67 kuhakikisha kama Sh. bilioni 100.5 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizo zimetumika vizuri.

Taarifa iliyotolewa jana na ofisi hiyo, ilieleza kuwa serikali ya awamu ya tano imejenga hospitali 67 nchini na mkoa wa Rukwa umejengewa hospitali tatu za wilaya zilizotembelewa na Nyamuhanga.

Katibu Mkuu huyo ametembelea na kujionea maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kalambo, unaotekelezwa katika mji mdogo wa Matai na tayari Sh. bilioni 1.5 zimepokewa, lakini hakuridhishwa na ujenzi wa hospitali hiyo.

"Kwa halmashauri ambazo fedha hizi zitakuwa hazijatumika vizuri, kwa kweli tutachukua hatua na katibu tawala wa mkoa kama nilivyoagiza jana, najua kuna vifaa ambavyo tayari vimeshanunuliwa pale ambavyo bado havijawekwa, uhakikishe kwamba kazi hiyo inaendelea ili vifaa hivyo vikishawekwa tuvitathmini," aliagiza.

Aliongeza kuwa Halmashauri ya Kalambo imetaja mahitaji ya Sh. milioni 700 ili kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo, jambo ambalo hakukubaliana nalo kutokana na tathmini iliyofanywa ya mahitaji ya fedha walizotoa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizo kuwa yangebaki mambo machache ambayo yasingeweza kuzidi Sh. milioni 300. Aliagiza kupewa maelezo ya kina kutoka kwa halmashauri hiyo ambayo ujenzi wa hospitali yake umefikia ukamilifu wa asilimia 76, kiwango ambacho alidai ni cha chini.

Alibainisha kuwa Aprili mwaka huu, Ofisi ya Rais Tamisemi ilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya upanuzi wa Zahanati ya Kijiji cha Samazi katika halmashauri hiyo na zahanati hiyo inapandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya, lakini amesikitishwa na malumbano yanayoendelea katika kijiji hicho juu ya eneo la ujenzi wa kituo hicho na hivyo kukwamisha ujenzi huo.

"Ofisi ya Rais Tamisemi imetoa maelekezo kwamba upanuzi ufanyike katika eneo la zahanati, iliyopo iongezewe majengo ili kiwe kituo cha afya cha Samazi.

"Tusiendelee na malumbano tena, tumeshatoa uamuzi kwamba upanuzi ufanyike pale kwenye zahanati ili tukipandishe hadhi kiwe kituo cha afya, tunategemea kazi hiyo ianze mara moja na ikamilike ndani ya miezi mitatu," aliagiza.


**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**

TANESCO
We light up your life

**TAARIFA KWA UMMA**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina watangazia wateja wake wote zikiwemo Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya umma, Viwanda na watu binafsi wenye madeni ya bili za umeme kuwa;

TANESCO inaendesha zoezi maalum la kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wote wanaodaiwa bili za umeme.

Wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka adha ya kusitishiwa huduma ya umeme katika msimu wa sikukuu.

**TANESCO HAITATOA TAARIFA NYINGINE ZAIDI YA TANGAZO HILI.**

**Imetolewa Na:**
**OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**
**18 Disemba2019**




Mratibu wa Vipindi wa EATV, Sophia Proches ( kulia), akimkabidhi zawadi Mkuu wa Idara ya Wateja wa Rejareja wa Benki ya I & M, Lilian Mtali, baada ya kumaliza mahojiano kuhusu huduma zitolewazo na Benki hiyo, kupitia kampeni ya Kibiashara Zaidi. . **PICHA: EATV**

# Wadaiwa sugu umeme kuonja joto la Tanesco

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme (Tanesco) limetangaza kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wake ambao ni wadaiwa sugu.


Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa jana na Ofisi ya Uhusiano wa Umma Tanesco Makao Makuu, wateja wote, zikiwamo taasisi za serikali na binafsi, mashirika ya umma, viwanda na watu binafsi, wenye madeni ya bili za umeme, watakumbwa na operesheni hiyo.

Katika taarifa yake hiyo, Tanesco ilieleza kuwa wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka kukatiwa umeme msimu huu wa sikukuu.

"Tanesco haitatoa taarifa nyingine zaidi ya tamko hili, hivyo wadaiwa wote wajitahidi kulipa bili za umeme wanazodaiwa kabla hawajasitishiwa huduma," Tanesco ilitahadharisha kupitia taarifa yake.

Ilielezwa zaidi katika taarifa hiyo kwamba Tanesco itaendelea kuendesha opereseheni hiyo ya kusitisha huduma ya umeme kwa wadaiwa wote watakaokaidi agizo lake hilo.

Ripoti za miaka ya karibuni za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zimekuwa zikilitaja shirika hilo kuwa miongoni mwa taasisi mbili za umma (pamoja na Jeshi la Polisi) zenye madeni makubwa huku pia zikiongoza kwa kufanya ununuzi wa gharama kubwa.




# Sababu kupigwa kalenda mahojiano ya Bulaya kortini

**Na Hellen Mwango**

MAHOJIANO katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kati ya upande wa Jamhuri na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, yamepigwa kalenda mpaka Desemba 23, mwaka huu atakapowasilisha hati yake ya kusafiria mahakamani.

Mbali na ubunge, Bulaya ambaye ni mshtakiwa wa tisa, upande wa Jamhuri ulisitisha kumhoji Desemba 6,mwaka huu katika shahidi wake baada ya kutakiwa kuwasilisha mahakamani hati yake ya kusafiria.

Kesi hiyo inasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na

INAENDELEA UK. 8

# Muuguzi atuhumiwa kumbaka mjamzito akisubiri kujifungua

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

MUUGUZI wa Kituo cha Afya Mamba, wilayani hapa, Abednego Alfred (32), anadaiwa kumbaka mjamzito aliyekuwa kwenye chumba cha kujifungulia, akisubiri kujifungua.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 18, saa mbili usiku, katika kituo hicho cha afya.

Alisema siku ya tukio, mwanamke huyo alipatwa na uchungu na kwenda kupata huduma ya kujifungua kwenye kituo hicho cha afya huku akiwa amesindikizwa na mama yake mzazi.

Alisema mjamzito huyo alipokelewa kituoni hapo na mtuhumiwa huyo ambaye alikuwa zamu kwenye wodi hiyo ya kujifungulia. Kamanda Kuzaga alieleza, wakati mtuhumiwa akimpatia huduma ya uzazi mgonjwa, alihisi hali isiyo ya kawaida katika sehemu zake za siri hali iliyomfanya ashtuke.

Alieleza kuwa mgonjwa huyo alijiinua na kumuona muuguzi Alfred akiwa anamwingilia katika sehemu zake za siri bila kujali hali aliyokuwa nayo.

Kamanda aliendelea kueleza mgonjwa baada ya kuona hivyo, aliinuka kitandani na kwenda moja kwa moja kutoa taarifa kwa mama yake mzazi (jina linahifadhiwa) ambaye naye alitoa taarifa kwa uongozi wa kituo hicho cha afya.

Vile vile, Kamanda alisema mtuhumiwa baada ya kufanya kitendo hicho aliondoka ndani ya chumba hicho cha kujifungulia na kisha kukimbia na kutokomea kusiko julikana. Hata hivyo polisi kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kumkamata.

Alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kushikiliwa na anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

# Makandarasi miradi 159 hatarini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeagiza makandarasi wote waliotekeleza miradi ya maji 159 nchini ambayo imekamilika lakini haitoi maji na iliyojengwa chini ya viwango, wachukuliwe hatua kali ikiwamo kutopewa tena tenda serikalini.

Hatua hizo pia zimeelekezwa kwa makandarasi ambao miradi imechukua muda mrefu kukamilika, hivyo kuisababishia hasara serikali.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa Sekta ya Maji Tanzania Bara.

Alisema kuna miradi 159 ambayo ni chechefu kutokana na kukamilika lakini haitoi maji na mingine inachukua muda mrefu kukamilika.

"Sehemu nyingine unakuta mradi umejengwa chini ya kiwango na watalaamu wa maji wapo, lakini ukiuliza utagundua kuwa fedha zimeliwa kwa kugawana mtalaamu wetu na mkandarasi," alisema. Naibu Waziri huyo alisema wakati wa kufanya miradi ya maji kuwa kichaka cha kuiba fedha, umekwisha na atakayegundulika hataonewa huruma.

Aliwataka wakurugenzi na watalaamu wa wizara kufuatilia miradi hiyo 159 ambayo ni chechefu na kuwachukulia hatua watalaamu wote waliohusika kuhujumu fedha za serikali. Alisema miradi 153 ipo vijijini na mingine sita iko mijini.

"Niwaombe sasa, tutoke maofisini twende kuangalia mitandao ya maji kama ni imara na mara nyingine taarifa zinakuja lakini mnachukua muda mrefu kutengeneza," alisema. Awali, akizungumzia hali ya upatikanaji wa maji nchini, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Kitila Mkumbo, alidai ni nzuri, akibainisha kuna takriban mita za ujazo bilioni 126 za maji huku mahitaji yakiwa ni mita za ujazo bilioni 40.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine, una lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya nusu mwaka 2019/2020 na kujipanga kwa ajili ya bajeti ijayo ya 2020/2021 ambayo ni ya mwisho katika awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano.

## Prof. Mbarawa akwama kutoa ushahidi kesi udanganyifu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, jana ilishindwa kusikiliza ushahidi wa Jamhuri wa Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, baada ya mshtakiwa Wilfred Massawe kuruka dhamana dhidi ya kesi ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Hata hivyo, mahakama hiyo imetoa hati ya kukamatwa mshtakiwa huyo ambaye pia ni mfanyabiashara wa jijini Dar es Salaam.

Hati hiyo ilitolewa na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali, Janeth Magoha, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa Jamhuri kutoka kwa Waziri Mbarawa, na kwamba walikuwa tayari kuendelea.

Hata hivyo, Magoha alidai mshtakiwa Massawe hakufika mahakamani bila taarifa, hivyo upande wa Jamhuri uliomba hati ya kukamatwa.

"Mheshimiwa hakimu, kwa kuwa mshtakiwa hajafika mahakamani na hakuna taarifa yoyote, Jamhuri tunaona anachelewesha kesi...shahidi wangu ana majukumu mengi ya kitaifa, hivyo tunaomba hati ya kukamatwa kwa mshtakiwa na tunaomba mahakama imuonye shahidi," alidai Magoha.

Hakimu Ally alisema mahakama imemuonya shahidi wa Jamhuri na kumwagiza afike mahakamani Januari 14, 2020.

Pia, ilitoa hati ya kukamatwa Massawe kwa kuruka dhamana pamoja na wadhamini wake kufika mahakamani.

Katika kesi ya msingi, Massawe anakabiliwa na mashitaka manne ikiwamo ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kujifanya yeye ni Prof. Mbarawa, kipindi hicho akiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mashtaka mengine yanayomkabili ni kujitambulisha kwa Waziri Kindamba, ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL) kuwa ni Prof. Mbarawa.

Katika kesi hiyo namba 3/2017, Massawe anadaiwa Novemba 25, 2016 akiwa maeneo ya Yombo Buza Temeke jijini Dar es Salaam, alijitambulisha kwa Alfred Samson kwamba ni Prof. Makame Mbarawa.

Katika shitaka la pili, inadaiwa Novemba 26, mwaka na mahali hapo, Massawe alijitambulisha kwa Izack Mwawima kuwa yeye ni Prof. Mbarawa.

Inadaiwa mshtakiwa huyo pia alijitambulisha kwa Waziri Kindamba kuwa ni Prof. Mbarawa.

TCCIA Investment Public Limited Company

TCCIA INVESTMENT PLC
P. O. Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania Tel: 255 – 22 – 276 0172/276 1725 Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvest.co.tz, Web site: http://www.tcciainvest.co.tz

NEW CEO ANNOUNCEMENT

The Board of Directors of TCCIA Investment PLC is pleased to announce the appointment of Mr. Peter William Kifunguomali as new CEO with effect from 1st January 2020 to succeed Mr Donald Kamori who is retiring at the end of December 2019 after serving the Company as its Chief Executive Officer for a period of fifteen years.

The Board appreciates maximum collaboration given by Mr Kamori to ensure a smooth transition

and handing over of leadership to his Successor. Also the Board would like to welcome onboard the new Chief Excretive Officer of TCCIA Investment PLC, Mr. Peter William Kifunguomali. The Board has confidence in him and trusts in his qualification and experience to deliver greater heights.

Mr Kifunguomali (38) started his career at Ministry of Natural Resources and Tourism, NBC Bank, LAPF Pensions Fund. Prior to his current role he was Head of Planning Section with the Public Service Social Security Pensions Fund (PSSSF) since September 2018 and also sat on the Company Board from July 2017 to June, 2019. Mr Kifunguomali holds a Master's Degree in International Business from Jamia Millia Islamia, New Delhi in 2014, Bachelor of Science in Economics, Project Planning and Management from Mzumbe University in 2007. He is also Alumni of St James Seminary where he pursued his secondary education.

Mr Kifunguomali's expertise is mainly in Project Planning, Development and Management. He has been part of a team involved in major projects in conducting performance analysis and feasibility studies. He has been also involved in preparation of project analyses, appraisals, detailed feasibility studies and capital budgets, analysis of short and long term investment in Government Securities and equities.

On behalf of the Board, I would like to congratulate Mr. Kifunguomali on his new role with TCCIA Investment PLC, and extend our deepest gratitude to Mr. Kamori for his leadership as CEO since January 2005.

Fortunatus M. Magambo
Board Chairman

215561702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutizame sheria kuokoa watoto 800,000 mitaani

**UNYANYASAJI** kijinsia unaohusisha kutelekeza familia, vipigo, watoto kuozwa, kupewa mimba na kugeuzwa kuwa wakazi wa mitaani ni jambo lililoibuka wiki hii kwenye mjadala ulioibua taarifa kuwa takribani watoto 800,000 wanaishi katika mazingira magumu au mitaani.

Tunashukuru kuwa kasoro za kisheria ni moja ya matatizo yanayochangia matatizo kwa watoto kwa mfano, sheria ya kutunza mtoto inazungumzia zaidi kumtunza mtoto lakini haimjali mama anayetelekezwa.

Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009, sura ya 4(2) inasema kuwa maslahi ya mtoto yatakuwa ndiyo msingi wa kuzingatiwa katika masuala yote yanayohusiana na mtoto. Aidha, yatakuwa yanashughulikiwa na taasisi za umma au taasisi za binafsi za Ustawi wa Jamii, mahakama au mamlaka za kiutawala. Sheria hii haijamgusa mama ambaye ni mzazi wa mtoto.

Sura ya 26:1(a),(b),(c) inaongelea haki ya mtoto wazazi wanapotengana, upungufu unaoonekana hapa ni kwamba , mama anayetelekezwa, pamoja na mtoto wake hawajahusishwa moja kwa moja kisheria. Inakuwa kama sheria haimfahamu mama mzazi, ndiyo maana inahitaji kufanyiwa marekebisho ili mama na familia inapotelekezwa kuwe na sheria za kumuwajibisha na kumwadhibu baba anayehusika na uvunjaji wa sheria ya kukataa familia yake inayomtelekeza mototo ambaye huishia mitaani.

Huenda kwa kutumia mwanya au udhaifu huo wanaume hupuuza kuwatunza watoto na hata kama wataitwa kwenye mashauri ya ustawi wa jamii hawaitikii wito na hawajali kutelekeza wanawake na watoto wao. Kutelekeza watoto takribani 1,000,000 na kuwaacha waishi mitaani ni jambo ambalo serikali inatakiwa kulitafutia ufumbuzi haraka. Kama suala ni sheria zirekebishwe ili kuzuia idadi hiyo isiongezeke.

Pamoja na vipengele vya sheria ya ndoa vinavyohusu umri wa kuolewa kufutwa na mahakama ya rufani, kuna haja pia ya sheria hiyo inapoandaa vipengele vipya vya kuiboresha itoe utaratibu wa ndoa za kimila ambazo nazo zina masuala yanayotatiza hatma ya watoto. Mara nyingi ndoa za kimila ni kama zinafanyika kwa utaratibu holela hivyo kuna haja ya kuuchunguza na kuuboresha kwa ajili ya ustawi wa watoto na mama zao.

Tunaiomba serikali kuzitazama ndoa za kimila ambazo mara nyingi zinasababisha familia kushindwa kutunza watoto ambao wengine huishia mitaani.

Hata hivyo, zama hizi kuna utaalamu na teknolojia ya kupima vinasaba polisi wanaweza kuutumia kutambua familia na wazazi wa watoto hao wanaoishi mitaani.

Tunaamini huu ndiyo wakati wa kufikiria namna ya kutumia kipimo cha DNA na kupata utambuzi wa watoto ili kuwawajibisha wazazi au walezi wa jeshi kubwa la watoto karibu 1,000,000 wanaoishi mitaani. Tunashangaa na kusikitika kusikia kuwa serikali inatumia mabilioni kila mwezi kusomesha wanafunzi elimu ya msingi hadi sekondari wakati watoto wengine karibu milioni moja wanakosa huduma hiyo na wanaishi katika mazingira magumu.

Tunaona kuwa kuna haja ya kuitazama pia sheria ya mahusiano kazini ya 2004 ili kuondoa eneo la kuwanyanyasa watoto hasa mabinti na kusababisha kupata mimba wakiwa watumishi wa ndani ambao pia watoto wao huishia kuishi mitaani.

Sheria ya kazi ya 2004 inaruhusu watoto wenye miaka 14 kupata ajira na kufanyakazi nyepesi, lakini binti wa miaka 14 au 15 anapokuwa mtumishi wa ndani hunyanyaswa kupindukia.

Ajira haramu kama hizi zinatakiwa pia kumulikwa na sheria kwa vile huchangia kuongeza watoto wa mitaani ambao idadi yao sasa inaelekea kufikia milioni. Tunaona kuwa sheria hizi zikitazamwa upya zinaweza kupunguza unyanyasaji watoto na kusababisha madhila kama kuishi kwenye mazingira magumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu duni, uzembe chanzo kikubwa janga ajali pikipiki

**USAFIRI** wa bodaboda upo takribani kila kona ya nchi na umekuwa ukitumiwa na watu mbalimbali.

Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambako bodaboda hizo zilianza mbali zaidi, nikiutaja mkoa jirani wa Kagera, hasa mjini Bukoba.

Usafiri wa bodaboda umekuwa ukitumiwa na watu mbalimbali ukiwawezesha watu kufika kwa urahisi katika maeneo waendayo, kwani hayapotezi muda katika foleni, hasa katika maeneo ya mijini.

Usafiri huo, pia umekuwa ukitumiwa na baadhi ya wazazi kwa kuwapeleka watoto shule, kutokana na wengi kushindwa kulipia usafiri wa mabasi ya shule.

Katika kufuatilia, nimebaini jambo moja kwamba, madereva wanaoendesha bodaboda, wengi hawana elimu inayojitosheleza kwa ajili ya kutumia vyombo hivyo.

Serikali imekuwa ikizungumzia hilo kila mara, kwamba kila anayetumia usafiri wa aina yoyote, ni lazima azingatie sheria, itakayomuwezesha kufika safari yake salama, katika sehemu aendayo

Kuna baadhi ya watu wanaovunja sheria kupitia vyombo vyao na wanapokamatwa, wanajihisi sheria imewaonea, wakati katika ukweli si sahihi, bali inakuwa kinyume chake.

> **Kuna baadhi ya watu wanaovunja sheria kupitia vyombo vyao na wanapokamatwa, wanajihisi sheria imewaonea, wakati katika ukweli si sahihi, bali inakuwa kinyume chake.**

Mtu anapoambiwa anapoanza safari yake, baadhi ya mambo ya msingi kama vile kufunga mkanda ni ya kuzingatia.

Pia, hata wale wenye watoto wanatakiwa wawaweke katika viti vyao, lengo ni kuwanusuru na uwezekano wa madhara safarini, hasa pale ajali inapotokea.

Lakini, mtu akiangaliwa katika magari binafsi, baadhi yake hazingatii hilo, watoto hayo wanakalishwa kwenye viti vya mbele na hawana vizuizi vyovyote.

Hapo ajali ikitokea mtoto kupona ni shida.

Ukija upande wa bodaboda ambao nazungumzia ni kila bodaboda ibebe abiria mmoja na kuwapo kofia ngumu mbili za dereva na abiria wake

Lakini, cha kushangaza unakuta baadhi ya bodaboda hawazingatii hilo na kuamua kufanya watakavyo wao.

Unakuta abiria wapo watatu katika bodaboda na aliyevaa kofia ngumu ni dereva pekee je ajili inapotokea nani wa kulaumiwa.

Kwa nini sheria tunazivunja wenyewe,wakati tunajua bodaboda moja inabeba mtu mmoja? Tujue, bila ya

kufuata sheria za usalama barabarani, bodaboda zitaendelea kusumbua na kuifanya serikali iingie gharama kubwa kuhudumia majeruhi ikiwamo matumizi makubwa ya damu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya kimataifa ya Masuala ya Usalama Barabarani, Fotunatusi Sokoni, anatoa mfano ajali za pikipiki kwa miaka miwili tofauti, zilisababisha jumla ya vifo 2,953.

Anaainisha, mwaka 1997 zilisababisha vifo vya watu 990 na majeruhi 1,997; huku mwaka 2017 kulitokea 1,584 zilizosababisha vifo 763 na majeruhi 1,224.

"Ukiangalia mwaka 2016 na 2017 kuna tofauti ya ajali 1,019, yaani zilipungua kwa kiwango cha asilimia 22.9 na waliojeruhi ilikuwa ni pungufu ya watu 773 katika kipindi hicho," anasema.

# Makosa ya jinai yapungua kwa 2%

Na Peter Mkwavila, DODOMA.

JESHI la Polisi nchini limesema kuwa makosa makubwa ya jinai yamepungua kwa asilimia 2.0 ambapo ni sawa na makosa 1,082 kwa kipindi cha Januari hadi Novemba 2019, ambapo yalikuwa 53,685,huku mwaka 2018 yalikuwa makosa 54,867.

Pia ajali za barabarani zimepungua kwa asilimia 26.2,ambapo mwaka 2018 majeruhi walikuwa 3689 na mwaka 2019 majeruhi 2722 .

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ambapo alisema kuwa asilimia 75 ya ajali zinasababishwa na uzembe wa binadamu.

"Hii ni hatua kubwa hivyo Jeshi la Polisi linaendelea kutoa wito kwa wananchi na wadau wote waendelee kutoa ushirikiano kwani swala la ulinzi na usalama ni letu sote,"alisema Misime.

Akizungumzia jeshi lilivyojipanga katika kuelekea kipindi cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2020, alisema kuwa nchi ni shwari na inaendelea kuwa ya amani, utulivu na usalama, nkusema kuwa ushwari huo umetokana na na ushirikiano mkubwa ambao Jeshi la Polisi linaendelea kupata kutoka kwa wananchi na kuwezesha uhalifu wa kijinai na ajali za barabarani kuendelea kupungua.

"Niwafahamishe kwamba Jeshi la Polisi maeneo yote tumejipanga ipasavyo kuzuia na kupambana na uhalifu na wahalifu katika kipindi hiki, kwani doria za miguu, magari, helikopta, pikipiki, mbwa na farasi katika mikoa na vikosi vyote zimeimarishwa ili kuhakikisha maandalizi na kusherehekea kunafanyika kwa amani, utulivu na usalama," alisema.

Aidha, alisema kuwa kinachotakiwa ni ushirikiano kutoka kwa wananchi hususani katika kuzuia kwani kwa kufanya hivyo kwa pamoja watakuwa wanawanyima wahalifu fursa ya kutenda uhalifu waliokusudia, na kusema kuwa wahalifu wanaishi ndani ya jamii kwani anaweza kuwa mwanafamilia, ndugu, rafiki, jirani au mkazi wa eneo moja.

"Tukishirikiana kupeana elimu juu ya ubaya wa uhalifu, kuchukia uhalifu na kuishi kwa uadilifu tutakuwa tumeshirikiana sote kuzuia uhalifu," alisema.

Vile vile, Misime alisema jeshi hilo linatoa wito na kusisitiza kila mmoja kutii sheria bila kushurutishwa kwani atakayekiuka wamejiandaa katika nyanja zote kumshughulikia mtu kama huyo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na asiwepo wa kumlaumu.

"Kila mmoja ajihadhari kuwa chanzo cha kuvunja sheria kwani hata onewa huruma atashughulikiwa ipasavyo"alisema.

Aliwataka wamiliki wa maeneo ya sherehe kuzingatia sheria na taratibu walizopewa katika maeneo yao za kuhakikisha usalama unakuwepo, jeshi la polisi linataka wageni na wananchi wote wafanye maandalizi na washerekee sikuu hizo kwa amani, utulivu na usalama.

"Ndiyo maana tumesema tumejiandaa ipasavyo kuwashughulikia wale wachache watakao jaribu kuvunja sheria yoyote iwe inayohusiana na jinai au usalama barabarani", alisema misime.

Pia aliwaonya watu wanaokwepa kusafiri mchana na badala yake kusafiri usiku kwa kudhani kuwa kwa kufanya hivyo wanakwepa mkono wa sheria.

"Jeshi la polisi linatoa wito kuwa hata kama mtu atasafiri usiku anatakiwa kuzingatia sheria, kuthamini maisha yake, familia yake na wategemezi wake," alisema.




## JKCI yatumia bi. 2/- kulipa gharama

Na Joseph Mwendapole

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), imetumia zaidi ya Sh. bilioni 1.2 kwa mwaka 2019 kwa ajili ya kulipa gharama za matibabu ya moyo kwa wagonjwa wanaotoka katika familia maskini na wasiokuwa na uwezo wa kulipia gharama hizo.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Agnes Kuhenga wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea msaada wa vifaa tiba pamoja na dawa kutoka Ubalozi wa China kupitia Timu ya madaktari kutoka nchini humo wanaofanya kazi hapa nchini.

Agnes alisema asilimia 10 hadi 15 ya wagonjwa wanaotibiwa katika Taasisi hiyo hawana kadi za bima ya afya na hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu na kwamba wagonjwa wa aina hiyo wanapata huduma za matibabu kwa Taasisi kugharamia matibabu yao.

"Januari mwaka huu hadi siku hii ya leo (jana) tumetumia zaidi ya Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa ambao hawakuwa na uwezo wa kuchangia gharama za matibabu. Ninaiomba mifuko ya bima za afya iweze kutoa elimu kwa Watanzania ili wajiunge na bima hizo ambazo zitawapunguzia wananchi gharama ya kulipia fedha za matibabu pindi watakapougua", alisema Agnes.

Agnes aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya watu wa China kwa misaada mbalimbali ya huduma za afya wanayoitoa katika Taasisi hiyo na kwa upande wa vifaa tiba pamoja na dawa walizozitoa alisema zitatumika kwa wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kuchangia gharama za matibabu.

Kwa upande wake,

INAENDELEA UK. 8

## JKCI yatumia bi. 2/- kulipa gharama

INATOKA UK. 7

mwakilishi wa Balozi wa Jamhuri ya watu wa China hapa nchini Yuan Lin alisema msaada wa vifaa tiba pamoja na dawa walizozitoa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kupitia madaktari wa Kichina wanaofanya kazi hapa nchini unathamani ya Sh. milioni 15.

"Ninaamini msaada huu ambao ni moja ya kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na China katika sekta ya afya utasaidia katika matumizi ya kila siku ya Hospitali na utachangia katika kutoa huduma ya matibabu kwa wagonjwa", alisema Lin. Naye Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Tiba Shirikishi, Dk. Delilah Kimambo alisema uhusiano wa Taasisi hiyo na Serikali ya watu wa Jamhuri ya China ulianza miaka mingi iliyopita ambapo hata Jengo la Taasisi hiyo lilijengwa kwa msaada wa Serikali hiyo.

Alisema Taasisi hiyo pia imekuwa ikipokea madaktari kutoka nchini China ambao wanatoa huduma za matibabu ya moyo pamoja na kufanya kambi maalum za matibabu ya moyo pia madaktari na wauguzi kutoka JKCI wanakwenda nchini humo kwa ajili ya kupata utaalamu zaidi wa magonjwa ya moyo.

## Maambukizi malaria yapungua

**Na Catherine Sungura,** DODOMA

Kiwango cha maambikizi ya ugonjwa wa malaria nchini kimepungua zaidi ya asilimia 50 ndani ya miaka miwili kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 kwa mwaka 2017.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, wakati wa kikao kazi cha kanda kinachojumisha,waganga wakuu wa mikoa, wilaya, wafamasia na waratibu wa malaria kutoka kanda tano za mikoa ya Dodoma, Singida, Njombe,Iringa na Morogoro.

Dk. subi alisema mkutano huo una lengo la kutathmini utekelezaji wa shughuli za malaria kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP).

"Tumedhamiria kuitokomeza na kuondoa kabisa malaria Tanzania na mafanikio yameanza kuonekana kwa kipindi cha miaka kumi sasa kwani mwaka 2010 kiwango cha malaria kilikuwa asilimia 18, lakini hivi sasa tunaongelea asilimia 7.3," alisema.

Amesema vifo vitokananvyo na malaria navyo vimepungua kwa zaidi ya asilimia 75 kwa zaidi ya miaka kumi, na vile vile watu wanaougua malaria na maambukizi mapya nao wamepungua kwa zaidi ya asilimia 67.

"Lakini Tanzania bado tunatajwa kama nchi yenye kiwango kikubwa chenye malaria katika nchi za Afrika mojawapo kati ya nchi kumi, ila bado tunayo fursa ya kuiondosha malaria nchini," aliongeza.

Aidha, Dk. Subi alisema kama kwa sasa wanataka kuwa na mpango endelevu wa kuondoa malaria ambao utasaidia kuondosha ugonjwa huo kuanzia viluilui pamoja na mbu wapevu.

## Aliyetimuliwa UDSM awatuliza wanafunzi

INATOKA UK. 2

wamepata stahiki zao, jambo tulilopigania," alisema.

Juzi uongozi wa UDSM ulitangaza kuwasimamisha masomo wanafunzi na viongozi watano wa serikali ya wanafunzi kwa kile ulichoeleza kuwa ni kuvunja kanuni na sheria za chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini.

Kusimamishwa kwa wanafunzi hao kulikuja siku moja baada ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kutoa saa 24 kwa uongozi wa UDSM kueleza hatua ulizochukua dhidi ya wanafunzi waliotishia kuandamana huku wakitoa saa 72 kwa HESLB kuwapa madai ya mikopo na stahiki nyinginezo.

Awali, wanafunzi hao walitoa tamko la kutishia kuandamana Desemba 19, mwaka huu, kushinikiza bodi hiyo kuwapa mikopo wanafunzi kwa kuwa toka vyuo vimefunguliwa, hawajapata fedha yoyote, hali inayowafanya waishi kwa shida.

## Mbowe atangaza dawa wasaliti wa Chadema

INATOKA UK. 2

malengo yoyote binafsi au ya kadamnasi, akaona nia yake binafsi inazidi nafasi na uhalisia wa uwapo wa chama chetu, hakika tutampinga," Mbowe alionya huku akizungumza kwa upole na umakini mkubwa.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kukipenda chama chao kwa wivu mkubwa na kuonya wanaofikiri kukisaliti chama hicho kuwa watapingwa kwa nguvu zote.

**MATOKEO YA KURA**

Mbowe amefanikiwa kutetea kiti chake baada ya kupata kura 886, sawa na asilimia 93 dhidi ya mpinzani wake, Cecil Mwambe, aliyepata kura 59 (asilimia sita) huku kura tatu zikiharibika.

Wakati hali ni hiyo, Mbowe akisomba idadi hiyo kubwa ya kura, makamu wake upande wa Tanzania Bara, Tundu Lissu, naye alitikisa matokeo kwa kuchukua asilimia 98 pasipo kuwapo mkutanoni.

Katika uchaguzi huo, Lissu aliyewania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chadema Tanzania Bara, alipata ushindi wa kishindo wa kura 930, sawa na asilimia 98 licha ya kutokuwapo nchini na hivyo kulazimika kupiga kampeni kwa njia ya video, akimshinda mpinzani wake, Sophia Mwakagenda aliyepata kura 11.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Said Issa Mohammed aliyegombea peke yake, alipata kura 839 za ndiyo, sawa na asilimia 88.7 na kura 95 za hapana (asilimia 10) huku kura 12 (asilimia 1.3) zikiharibika.

Kumalizika kwa uchaguzi huo kumehitimisha rasmi mchakato mrefu wa uchaguzi wa ndani wa Chadema ulioanza mwezi Novemba 18, mwaka huu kwa ngazi ya viongozi wa kitaifa.

**PONGEZI ZA ZITTO**

Muda mfupi baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi huo, Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliwapongeza viongozi wapya wa Chadema waliochaguliwa katika mkutano mkuu wa chama hicho.

Zitto aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, akiwapongeza viongozi hao kwa kushinda katika uchaguzi huo, hasa Mbowe, aliyechaguliwa tena kuwa mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini. "Nakupongeza Freeman Mbowe kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chadema Taifa, tushirikiane kuweka mikakati ya pamoja kuhami demokrasia yetu," Zitto alisema.

Mwanachama huyo wa zamani wa Chadema pia aliwapongeza wanachama wa chama hicho kwa kumaliza mkutano mkuu na kuchagua safu ya uongozi kwa miaka mitano ijayo.

Aliwahakikishia viongozi hao kwamba, ACT iko tayari kuendelea kushirikiana na Chadema na viongozi wengine wa upinzani katika harakati za kuiendeleza demokrasia nchini.

***Imeandikwa na Enock Charles na Maulid Mmbaga**

## Wadhamini wabanwa kumpeleka Lissu makamani vinginevyo...

INATOKA UK. 3

Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

## Sababu kupigwa kalenda mahojiano ya Bulaya kortini

INATOKA UK. 4

jopo la mawakili sita wakiwamo, mawakili wa Serikali Wakuu, Paul Kadushi, Faraja Nchimbi, Pendo Makondo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali, Jaqline Nyantori na Salimu Msemo.

Upande wa utetezi, uliongozwa na jopo la mawakili watatu, John Mallya, Hekima Mwasipo na Fredy Kihwelo. Nchimbi alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili kuhojiwa na upande wa Jamhuri mshtakiwa Bulaya.

Hata hivyo, Mallya alidai kuwa upande wa utetezi hauko tayari kuendelea kwa sababu Wakili Peter Kibatala aliyewaongoza washtakiwa kutoa ushahidi amepata udhuru wa kifamilia akiwa katika viunga vya mahakama hiyo.

"Shahidi aliandaliwa na Kibatala, lakini amepata dharura ya kifamilia akiwa hapa eneo la mahakama... utaratibu wetu utetezi Kibatala aliwaandaa shahidi wa kwanza mpaka wa tisa na sisi mawakili wengine tutawaandaa mashahidi," alidai Mallya.

Akijibu hoja za utetezi, Kadushi alidai ni hatari kama mahakama ikijiingiza katika mtego wa utetezi kwamba kesi isiendelee na mahojiano kwa sababu mmoja wa mawakili katika jopo lao amepata dharura.

"Mheshimiwa hakimu, mimi nilimuandaa shahidi wa sita wa Jamhuri, Koplo Charles, lakini nilipopata udhuru mawakili wengine katika jopo la Jamhuri waliendelea na shahidi huyo hivyo hoja hiyo si ya kisheria itupiliwe mbali," alidai Kadushi. Alidai jambo la pili kuhusu amri ya mahakama iliyomtaka mshtakiwa Bulaya kuwasilisha hati yake ya kusafiria litekelezwe.

Hata hivyo, upande wa utetezi ulidai washtakiwa wamekesha kwenye mkutano, hawakupata nafasi ya kurudi nyumbani kwa sababu ya kuwahi mahakamani.

Hakimu Simba alisema amesikiliza hoja za pande zote mbili kesi hiyo itaendelea kusikilizwa Desemba 23, mwaka huu na Bulaya awasilishe hati yake ya kusafiria saa 2:30 asubuhi siku hiyo.

Awali Bulaya alidai siku ya tukio alikaribishwa kusalimia wananchi jukwaani, aliondoka eneo hilo kwenda Mbweni kujiandaa na safari ya kumsindikiza rafiki yake Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, kwenye matibabu Afrika Kusini.

Akihojiwa na Wankyo, shahidi huyo alidai Februari 16, 2018 alikuwapo katika viunga vya Buibui, na kwamba msherehesha ji wa mkutano wa kufunga kampeni, Meya wa Ubungo, Boniface Jacob alipomkaribisha jukwaani, alipanda na kuwasalimia wananchi.

Hata hivyo, ilipofika saa 11 aliongozana na Mdee kwenda nyumbani Mbweni, na kwa sababu alimweleza anaumwa alilazimika kusafiri naye Afrika Kusini kwa matibabu.

Mbali na Bulaya na Mdee, washtakiwa wengine ni Mwanyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe; Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vincent Mashinji; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya.

Pia wamo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashitaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, Dar es Salaam.

Kesi inaendelea leo kusikilizwa ushahidi wa utetezi.

HABARI KITAIFA

# JPM akumbusha shamba la baba yake lilivyotaifishwa

**Na Daniel Limbe,** CHATO

RAIS John Magufuli amekumbusha namna serikali ilivyotaifisha shamba la baba yake mzazi pasipo kulipwa fidia.

Shamba hilo lililoko Kijiji cha Mlimani, Kata ya Muungano wilayani Chato mkoani Geita, lilitaifishwa na serikali mwaka 1968 na hakuna malipo yoyote yaliyofanyika licha ya kuwapo mazao, miti na malisho ya mifugo. Rais Magufuli alikumbusha mkasa huo juzi wakati wa uzinduzi wa jengo la mahakama na ofisi ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji wilayani Chato ambazo zimejengwa kwenye maeneo ambayo awali yalimilikiwa na wananchi akiwamo baba yake mzazi, Joseph Magufuli.

"Bahati nzuri ofisi hizi zimejengwa eneo hili la Mlima ambao ninalifahamu vizuri sana... mimi nilichunga ng'ombe hapa, maana pale pembeni lilikuwa shamba la baba yangu.

"Serikali ililitaifisha mwaka 1968 na hakulipwa hata senti moja ya fidia. Mzee wangu alifuatilia sana haki yake, lakini alijibiwa kwa barua kutoka Ikulu kuwa ardhi ni mali ya taifa, kwa hiyo, hakupata chochote licha ya kwamba kulikuwa na mazao mbalimbali pamoja na miti," alisema.

Mbali na baba yake, Rais Magufuli aliwataja wazee wengine waliokuwa wakimiliki mashamba hayo kuwa Nikasi Mayala, Costantine Misungwi na mwingine aliyemtaja kwa jina moja la Tangawizi (wote marehemu).

Rais Magufuli aliipongeza Idara ya Mahakama kwa kujenga jengo kubwa la mahakama litakalosaidia kutoa haki kwa wananchi na kuwataka baadhi ya wananchi wanaodhani ujenzi huo umefanyika Chato pekee, kuondoa dhana hiyo kwa kuwa uboreshaji na ujenzi wa majengo ya mahakama unaendelea maeneo mbalimbali nchini.

"Wananchi walikuwa wakiteseka sana maana mahakama ya wilaya ilikuwa Biharamulo, wakati mwingine hata mahabusi walikuwa wanataabika sana kukaa gerezani zaidi ya miaka miwili pasipo kuletwa kwenye Mahakama ya Mwanzo Chato kusikiliza kesi zao kutokana na visingizio mbalimbali.

"Kwa hiyo, uwapo wa mahakama hii pamoja na gereza lililopo nyuma ya mlima huu itasaidia sana kupunguza msongamano wa mahabusi gerezani," alisema.

Awali alitoa taarifa ya utendaji wa mahakama nchini, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, mbali na kuipongeza serikali kwa kuongeza bajeti ya utendaji wa idara ya mahakama kila mwaka, alisema bado wanakabiliwa na uchakavu wa majengo ya mahakama katika baadhi ya maeneo nchini na baadhi ya majengo hayafai kabisa kutolea huduma za utoaji haki.

"Tunatambua kazi kubwa ulizozifanya kwa kuboresha majengo ya mahakama nchini maana ni muda mrefu sana idara ya mahakama ilisahaulika sana kiasi kwamba tuna majengo mengine hayafai hata kutolea huduma kutokana na uchakavu," alisema.



Baadhi ya wanachama cha wamiliki wa kampuni ya bima nchini (ATI), wakifurahia na Mkurugenzi wa Leseni na Usimamizi wa Mwenendo wa Soko kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Samwel Mwiru, wakati wa hafla ya kuaga Mwaka 2019 na kuukaribisha Mwaka 2020 jijini Dar es Salaam, juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Kesi kumwingilia mwenye ulemavu yapigwa kalenda

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa 'A' Chakechake, Pemba chini ya Hakimu Abdullarzak Abdaullkadir Ali, imeipiga kalenda kesi inayomkabili mtuhumiwa Abduraham Maulid Rashid, anayetuhumiwa kumwingilia mlemavu wa akili, kutokana na upande wa mashtaka kutopokea mashahidi.

Baada ya mtuhumiwa huyo kuwasili kortini, huku akiwakilishwa na Wakili Zahran Mohamed Yussuf, mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Mohamed Ali Juma, alidai kuwa shauri hilo lilitarajiwa kuwasikiliza mashahidi, ingawa hawajawapokea mashahidi.

Alidai mbele ya hakimu huyo kuwa kutokana na kutopokea mashahidi hao, ni vyema mahakama hiyo ikalipangia tarehe nyingine.

Baada ya Juma kukamilisha maelezo yake, ndipo hakimu alipomuuliza wakili wa mtuhumiwa kama ana dai lolote.

Wakili Yussuf, alimweleza hakimu kuwa hana pingamizi na maelezo ya upande wa mashtaka na kuiomba mahakama hiyo kulipanga shauri hilo hadi tarehe nyingine.

Hivyo hakimu huyo alisema shauri hilo litarudi tena mahakamani Januari 28, mwaka 2020, na kuagiza upande wa mashtaka kupeleka mashahidi siku hiyo.

Awali mwendesha mashtaka alidai mtuhumiwa huyo alimwingilia mwanamke mwenye ulemavu wa akili mwenye miaka 18, mkazi wa mjini Chakechake.

Ilidaiwa mtuhumiwa huyo alifanya tendo hilo Julai 27, mwaka huu, majira ya usiku eneo la Mtoni Chakechake.

Kufanya hivyo ni kosa kinyume cha kifungu cha 116 (1) cha Sheria ya Adhabu Namba 6 ya Mwaka 2018.

# Taasisi za bima zaombwa maeneo yasiyo na huduma

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za bima zimetakiwa kufika mikoa mbalimbali ambayo haijafikiwa na huduma za bima ili kuhakikisha inaondokana na uhaba wa huduma hizo kila sehemu kwa kutoa fursa zaidi kwa wakulima na watu wenye kipato cha chini.

Wito huo ulitolewa leo Desemba juzi na Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Kampuni ya Bima nchini (ATI), Khamis Suleiman, wakati wa hafla ya kuuaga mwaka 2019 na kuukaribisha mwaka 2020 jijini Dar es Salaam.

Khamis alisema mwaka 2020, Taasisi hiyo na Mamlaka husika imetenga bajeti kubwa kuhamasisha wananchi kupata elimu ya bima.

Aidha, alisema kuwa taasisi hizo zinapaswa kufika mikoa ambayo ina uhaba wa huduma za bima ili kuwa na uwiano sawa na mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya.

Alisema kazi kubwa ya Chama cha Wamiliki Bima kinahakikisha huduma za bima zinawafikia wananchi kwa gharama nafuu, pamoja na kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi ambao kwa sasa ni asilimia moja ya pato la Taifa na lengo ni kutoa asilimia tati katika miaka mitatu ijayo.

Alisema chama hicho kimepata mafanikio mwaka 2019 kwenye kusimamia bei sahihi za bima hizo kwa wananchi, kuzuia hasara kwa kampuni hizo, kuchangia kodi serikalini.

"Mwaka 2018 kulikuwa na changamoto nyingi sana, nafikiri mahesabu yatakuwa mazuri zaidi mwaka 2019, lakini changamoto bado zipo tunajitahidi kuzitatua changamoto hizo," alisema na kuongeza:

"Na changamoto kubwa ni elimu ya bima kwa wananchi hawaelewi kuhusu faida za bima, mwaka 2020 kutakuwa na mafanikio zaidi kuliko 2019."

Mkurugenzi wa Leseni na Usimamizi wa Mwenendo wa Soko kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), Samwel Mwiru, alisema wananchi wamezidi kuwa na hamasa katika huduma za bima mwaka hadi mwaka licha ya kuwa na uboreshaji kwenye hamasa hiyo.

Mwiru alitoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa kukata bima kwa manufaa yao, na kwamba Watanzania wana kila sababu ya kuchangamkia fursa hiyo kutokana na uwapo wa kampuni 32 za utoaji huduma za bima, madalali wanaotoa huduma hizo 130 na mawakala zaidi ya 600 kote nchini.

Alisema changamoto kubwa katika sekta ya bima, wananchi wengi hawana elimu kuhusu bima.

Alieleza kuwa TIRA na kampuni yana wajibu wa kuelimisha wananchi hao kuhusu umuhimu wa huduma hizo na kuwafikishia kwa njia mbalimbali.

# Halmashauri yapewa siku 90 za kituo afya

Na Gurian Adolf, KALAMBO

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamuhanga, ametoa siku 90 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa kuhakikisha inaanza ujenzi wa Kituo cha Afya, Samazi, vinginevyo itanyang'anywa fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Agizo hilo alilitoa hivi karibuni katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vituo vya afya pamoja na hospitari za wilaya katika mkoa wa Rukwa.

Alisema serikali ilitoa fedha muda mrefu kiasi cha Sh. milioni 400 kwa ujezi wa kituo hicho, lakini mpaka sasa ujenzi wake haujaanza, kitendo ambacho ni kuchelewesha huduma kwa wananchi. "Serikali imetoa maelekezo na sio muanze tena malumbano ya wapi kijengwe kituo hicho," alisema na kuongeza:

"Kama mtaendelea na hali hii mtanyang'anywa fedha hizo wapewe wengine wanaozihitaji, na wako tayari kutekeleza maelekezo ya serikali kwa wakati."

Katibu Mkuu huyo wa Tamisemi alielekeza kuwa kwa kuwa katika kijiji hicho kuna kituo cha afya, kisijengwe kipya badala yake kilichopo kipanuliwe ili kiwe na majengo mengi ambayo yatakidhi mahitaji ya sasa.

Nyamuhanga alifafanua kuwa kituo kilichopo kimeonekana ni kidogo kutokana na idadi ya watu waliopo wakati huu.

Aidha, alisema serikali inategemea kutoa fedha kiasi cha Sh. milioni 300 kwa kila hospitali ya wilaya kwa ajili ya kukamilisha ujenzi, na aliwaagiza wakurugezi nchi nzima kuzitumia fedha hizo vizuri ili zikidhi mahitaji.

Imeelezwa kuwa zaidi ya vituo vya afya 350 vipya vimejengwa nchi nzima, na vituo vingine 67 vinatarajiwa kujengwa ifikapo mwakani.



Mkazi wa Kijiji cha Masinono, Kata ya Bugwema, Musoma Vijijini mkoani Mara, Francis Owiya na familia yake, wakihudumia shamba lao la dengu, ambalo ni miongoni mwa mazao mapya ya biashara yaliyoanzishwa miaka ya hivi karibuni katika wilaya hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wahangaikia ujenzi vyumba 13 madarasa

Na Sabato Kasika

WILAYA ya Musoma mkoani Mara yenye halmashauri mbili, inatarajia kumaliza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari ifikapo Februari 15, mwaka ujao wa 2020.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka mjini Musoma jana, mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vencent Anney, alisema tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa lipo katika Halmashauri Musoma.

"Halmashauri hii yenye jimbo la Musoma Vijijini, ina uhaba wa vyumba 13 vya madarasa, juhudi zinafanyika ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo linaisha ifikapo Februari 15 mwaka ujao," alisema Dk. Anney.

Alisema, serikali kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika na wadau wengine wa elimu, wanaendelea na kazi ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba hivyo, ili wanafunzi wote waliofaulu mwaka huu waweze kuanza masomo.

"Wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka ujao ni 3, 498, lakini 619 kati yao watasubiri kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa ndipo waungane na wenzao," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, Musoma Vijijini ina sekondari 18 na kwamba nyungine zinaendelea kujengwa na huenda zikaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao.

Alizitaja sekondari mpya, ambazo ziko hatua za mwisho za ujenzi kuwa ni Mapigano Memorial na Busambara, kwamba zina vyumba vya kutosha vya madarasa, madawati na nyumba za walimu.

"Ujenzi wa shule hizi ukikamilika kabla ya Januari 15 mwaka 2020, utapunguza mrundikano wa wanafunzi madarasani uliopo kwenye sekondari za kata za jirani zisizokuwa na shule," alisema.

Alisema, wakazi wa kata Bugoji na Busambara wamedhamiria zianze kuchukua wanafunzi mwaka ujao, na kwamba madarasa ya kidato cha kwanza, madawati na ofisi za walimu.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, kinachoendelea sasa ni ujenzi wa vyoo vya wanafunzi na walimu, ambao utakamilika kabla ya Desemba 24, huku ujenzi wa majengo mengine muhimu nao ukiendelea.

# Waziri aagiza wataalamu andiko maporomoko kuwa chanzo maji

Na Frank Monyo, aliyekuwa MOROGORO

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amewataka wataalamu wa ndani wa Wizara wa Maji kuandika andiko la mradi litakalofanya maporomoko ya Ululu katika mto Mgeta wilayani Mvomero kuwa chanzo kikuu cha maji.

Maporomoko hayo yatamaliza kero ya muda mrefu katika Mkoa wa Morogoro na mikoa ya jirani. Alitoa maelekezo hayo alipotembelea na kukagua maporomoko hayo yenye urefu wa mita 1,500 kutoka usawa wa bahari ambayo ni chanzo kinachopeleka maji yake mto Mgeta ambao nao unamwaga maji yake mto Ruvu unaohudumia Pwani na Dar es Salaam.

"Huwa nasikitika sana kuona wananchi wa Morogoro na wilaya zake wanapata shida ya maji, niliwauliza wataalamu wetu wa ndani kwanini Morogoro kuna shida ya maji,?.. tunaona ongezeko la watu, tunaona ongezeko la viwanda haiwezekani shida hii, tuondokane na bwawa la Mindu tuhakikishe tunaandaa andiko linalokwenda kutatua tatizo la maji katika mkoa huu kwa kutumia maporomoko haya," alisema Aweso.

Alisema katika suala la utunzaji wa vyanzo vya maji, ofisa wa maji Bodi ya Bonde hilo, Simon Ngonyani, anastahili pongezi kwa kuhakikisha chanzo hicho kinalindwa, kutunzwa na kuwa endelevu kwani andiko litakapokamilika mradi huo utaanza kusaidia wakazi wa Kijiji jirani cha Bunduki na wakazi wa mkoa huo na jirani.

Ngonyani, alisema kufuatia ukubwa wa maporomoko hayo ana uhakika yatasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya maji katika Mkoa wa Morogoro na mikoa ya jirani.

Ngonyani, aliwakumbusha wamiliki wa viwanda kwenye ukanda wa Bonde la Wami Ruvu kuunganisha nguvu na kuchangia fedha kidogo katika utunzaji wa vyanzo vya maji na uhifadhi ili viendelee kuwapo kwa faida yao katika uzalishaji pamoja na vizazi vijavyo.

Naye Kaimu Meneja Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (Ruwasa), John Msengi, alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa mkoa huo wapo chini ya kiwango cha kiilani pamoja na malengo ya milenia kwani kwa mjini upatikanaji maji ni asilimia 77 na vijijini ni asilimia 69.

"Tunatakiwa ifikapo 2020 hali ya upatikanaji maji kwa mjini iwe ni asilimia 90 na vijijini iwe asilimia 85, kwa hapa Morogoro tatizo tulilonalo ni uwekezaji katika miundombinu kwani tumetoka kutembelea chanzo cha maporomoko ya Ululu katika mto Mgeta ambao utaisaidia kumaliza tatizo la maji katika wilaya ya Mvomero na Morogoro andiko litakapokamilika kwani maji ni mengi," alisema Msengi.

# DC awakanya viongozi CCM kuingilia watendaji

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, amewataka viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuacha kuingilia viongozi wa serikali wanapotekeleza majukumu yao.

Chaula alitoa onyo hilo hivi karibuni mkoani Manyara, wakati akizungumza kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema shida iliyopo Simanjiro ya migogoro ya ardhi haisababishwi na wananchi bali ni viongozi.

"Viongozi wa CCM watuache tufanye kazi, wakati mwingine wanatuingilia majukumu yetu, watuache tufanye kazi kutekeleza ilani yao,"alisema Chaula. Alisema changamoto wanayoipata wakati wanatekeleza majukumu yao hasa ya kutatua migogoro ya ardhi ni kuingiliwa na viongozi wa chama badala ya kuwaacha wakatekeleza majukumu yao.

Aidha, Chaula alisema katika kumaliza migogoro hiyo, amejipanga kuzunguka kata zote 18 za wilaya yake kutoa semina kwa viongozi wa serikali za vijiji ili wasaidiane kudhibiti migogoro hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti alikiri kuwa Wilaya ya Simanjiro na ya Kiteto zina migogoro mingi ya ardhi.

"Huko Simanjiro na Kiteto wakuu wa wilaya, nataka muwe wakali sana ikiwezekana muwe mnawakutanisha viongozi wa vijiji,"alisema Mnyeti.

Aidha, alisema wilaya hizo kuna migogoro ya ardhi ambayo viongozi wa vijiji wanauza maeneo ya wananchi bila wananchi kujua. Mbunge wa jimbo la Kiteto, Emmanuel Papian, alisema kwa kuwa viongozi wa vijiji waliokuwapo kabla ya uchaguzi wa hivi karibuni waliokuwa wanatafuna fedha za michango na kujenga urafiki na baadhi ya viongozi wa CCM, aliwashauri kutoendekeza urafiki huo.

"Nashauri nyie viongozi kama Mkuu wa Wilaya au Mkoa, msiogope kutimiza majukumu yenu na msiendekeze viongozi wa CCM wanaotaka kuona kuwa maslahi yao yanalindwa. Bali wakiharibu muwatimue ili watakaobaki wasonge mbele,"alisema Papian.



Kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jijini Dar es Saalam baadhi ya mito ilifurika mchanga na hivyo kutoa fursa ya ajira kwa vijana. Pichani vijana wakizoa mchanga na kwenda kuuza kando ya daraja la Mbezi Beach jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mwenyekiti mpya wa kijiji atema cheche

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

MWENYEKITI mpya wa Kijiji cha Mbuguni wilayani Arumeru mkoani Arusha, Hosea Palangyo, ameanza kazi na kuonya kuwashughulikia wananchi na wajasiriamali wasio na vyoo.

"Kwenye hili nitasimama kidete kwani kuna baadhi ya wafanyabiashara wenye baa, mama lishe, saluni hawana vyoo tutakula nao sahani moja ili wawe na vyoo bora tuepuke magonjwa," alisema Palangyo.

Palangyo aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wake wa kwanza wa kijiji tangu achaguliwe kuongoza kijiji hicho hivi karibuni.

Alisema wanakijiji hicho wanapaswa kufungua ukurasa mpya wa maendeleo kwa kupanda miti hiyo, kwenye taasisi mbalimbali za serikali ikiwemo shule, vituo vya afya na polisi.

Alisema kupitia kamati ya afya, mazingira na usafi wananchi wa kijiji hicho wanapaswa kutunza mazingira yao ikiwamo kila mfanyabiashara awe na eneo la choo.

Aliwataka wananchi wa eneo hilo, kuanza ukurasa mpya wakubadilisha mazingira yao kwa kupanda miti 100.

Mkazi wa Kijiji cha Mbuguni, Steven Melanyi, alisema japokuwa viongozi wa kijiji hicho ni wapya lakini wangepaswa kutoa idhini ya kujadili taarifa ya ujenzi wa madarasa ya shule ya sekondari Mbuguni.

"Ni kweli ninyi hamhusiki na matumizi ya fedha hizo ila wananchi wangeachwa wajadili fedha zao zilizochangwa na wao wenyewe kwani wana haki ya kujua matumizi ya namna ya fedha zao zilivyotumika," alisema Melanyi.

Mmoja kati ya wajumbe wa kamati ya ujenzi wa shule hiyo, Msafiri Mkali alisema walifanya kazi hiyo kwa kujitolea bila kulipwa na ukaguzi ulifanyika ikaonekana hakuna ufujaji wa fedha.

"Tunapaswa kupongezwa kwani tumefanya kazi yetu kwa uadilifu hivyo hatupaswi kubezwa kwani tulijitolea kwa hali na mali katika kusimamia ujenzi wa madarasa hayo hadi kufikia hapa tulipo,"alisema Mkali.

# Kijiji chanufaika bweni, nyumba bora za walimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAKIJIJI cha Khusumay wilayani Karatu wamenufaika na mradi wa bweni la wasichana na nyumba za walimu unaofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Kufuatia mafanikio hayo wameishukuru serikali na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaofanywa na Tasaf ulioiwezesha kuwajengea bweni moja la wasichana na nyumba mbili za kisasa kwa ajili ya familia nne za walimu wa Sekondari ya Baray.

Kazi hizo ziligharimu zaidi ya Sh. milioni 343.8.

Akizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Karatu Theresia Mahongo, Yustina Indoy, mwakilishi wa wanakijiji hicho, alisema kijiji kina kaya 430 zenye wakazi zaidi ya 2,000, hivyo kitendo cha kuimarisha shule hiyo, kutawainua wakazi hai wa pembenzoni kielimu.

Alisema kabla ya kujengewa bweni na nyumba hizo wanakijiji hicho walifanya mkutano na kuibua mradi huo ambao Tasaf iliutekeleza.

"Sisi wananchi tulichanga Sh. milioni 49.3 kati ya hizo na Tasaf alitoa milioni 294.4, lakini nasi tulijitolea nguvu zetu kama kubeba mawe na kusaidia kazi ndogondogo za mafundi,"alisema.

Alimwambia Mkuu wa Wilaya kuwa ujenzi wa bweni hilo umekamilika na wanafunzi wa kike waliopo kwa sasa ni 76 ambao mahitaji yao mabweni yametosheleza .

Alisema bweni hilo ni mkombozi kwa watoto wao wa kike ambao baadhi yao walikuwa wakitembea umbali mrefu kufika shuleni hapo na kukutana na vishawishi njiani vilivyosababisha kupata ujauzito na utoro.

Akiwajibu wananchi Mkuu wa Wilaya, Theresia Mahongo, aliwaomba wanakijiji hao na wanafunzi kutunza miundombinu ya shule hiyo ili isaidie wanafunzi wa vizazi vya sasa na vijavyo kupata elimu.

Mahongo alisema Tasaf imekomboa wananchi wake wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kwa kusaidia mambo mengi yakiwamo kuwakwamua kiuchumi baada ya kuwapatia fedha za kusaidia familia masikini.

"Sasa ninachotaka nyie wanafunzi hasa wa kike msiiangushe serikali ambayo imefanya juhudi hizi kupitia mpango huu, kuwajengea bweni safi, someni na achaneni na watu wanaowadanganya kwani wanaume hao watawakatisha ndoto zenu,"alisema.

## Serikali yawataka vijana kuanzisha miradi ya sura ya uchumi wa kati

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, amewataka vijana wilayani Siha, kujikita katika kuanzisha miradi ya kiuchumi inayoakisi sera ya Rais John Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na wa viwanda.

Ulega alitoa rai hiyo jana, wakati alipotembelea na kukagua miradi ya uzalishaji wa vyakula vya mifugo inayoendeshwa na kikundi cha vijana cha MKAF cha Wilaya ya Siha.

"Sera ya serikali ni kuibadilisha Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Ushiriki wa vijana katika kilimo na uzalishaji ni muhimu kufikia azma hiyo", alisema.

Alikipongeza kikundi cha vijana cha MKAF kwa kuanzisha mradi wa kutengeneza chakula cha mifugo kikiwamo cha ng'ombe wa maziwa.

Kwa mujibu wa Ulega, chakula hicho bora cha mifugo kinaongeza mnyororo wa thamani wa maziwa ya ng'ombe wa Tanzania.

"Mradi mzuri wa maziwa ni dhahiri utaboresha sekta ya mifugo nchini na hatua hii inaakisi dhana na dhamira ya Rais wetu Dk. John Magufuli ya kukuza sekta ya mifugo nchini ikiwamo kupata bidhaa bora zitokanazo na mifugo kwa ajili ya kuuza nje ya nchi", ailsema.

Aidha, Naibu Waziri Ulega pia aliwapongeza wadau mbalimbali wakiwemo SNV na Match Maker Associates (MMA) ambao alisema wanafanya kazi zinazohakikisha ya kuwa MKAF wanatimiza malengo yao wakati wakitekeleza miradi yao.

Awali, wakati akiwasilisha taarifa yake kwa Naibu Waziri Ulega, Katibu wa Kikundi cha Vijana cha MKAF, Alfred Peter, alisema kikundi hicho kilianzishwa baada ya vijana kushiriki mafunzo yaliyolenga kubaini fursa zilizoko kwenye mnyororo wa thamani wa Maziwa.

Akizungumzia changamoto wanazopitia katika kutekeleza majukumu yao, Peter alisema ni pamoja na upungufu wa ardhi ya kulima mimea ya ziada na ambayo alisema ndiyo malighafi kuu katika utengenezaji wa chakula cha mifugo.

"Hivi sasa tuna ekari tatu tu ikilinganishwa na ekari 30 ambazo tunahitaji kufikia malengo yetu ambayo tumejiwekea hadi sasa; tunaiomba serikali itusaidie kuboresha uzalishaji wetu na kuongeza fursa za kazi na mapato", alisema.

Wakati wa ziara hiyo, mbali na kutembelea mradi wa vijana wa kikundi cha MKAF, Naibu Waziri Ulega pia alikagua mradi wa ATM ya maziwa pamoja na wa maziwa ya Nronga Women Group kikundi kilichoko wilayani Hai pia.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akihutubia wageni waalikwa wakati wahafla ya Tuzo ya mwaajiri bora wamwaka 2019 iliyoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) katika Hotel ya Serena jijini Dar es Salaam juzi hafla hiyo iliyoudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, na wenye Ulemavu, Stella Ikupa pamoja na Taasisi mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahoji iko wapi serikali watoto wakicheza kamari?

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

JUKWAA la vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) la Wilaya ya Siha, limehoji sababu za serikali kukaa kimya badala ya kudhibiti watoto wanaoshiriki michezo ya kubahatisha maarufu kama korokoro.

Tamko la wanaharakati hao wilayani humo lililotolewa jana, idadi ya watoto wanaocheza kamari ya korokoro katika miji midogo ya Sanya Juu na Kirua (Lawate) inahatarisha hatima yao kimasomo.

Mwenyekiti wa Tapo Christina Kavishe, alisema ukimya wa serikali ya Wilaya ya Siha, kudhibiti watoto kushiriki korokoro, ndio uliowafanya kujitokeza hadharani kukemea kucheza mchezo huo, kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Akieleza namna watoto wanavyotoroka shuleni na kwenda mtaani kucheza mchezo huo, mmoja wa wazazi, Victoria Mbando mkazi wa Kirua, alisema aligundua mwanaye anacheza korokoro baada ya kumkamata na Shilingi 6,000 mfukoni.

"Nilimkuta na 6,000 baada ya kumpekua, nilipomchapa na kumtaka aniambie kazipata wapi, ndio akasema anacheza korokoro," alisema Mbando.

Jukwaa hilo lipo chini ya mradi wa majaribio wa mwaka mmoja wa nguvu ya pamoja katika kupambana na ukatili wa kijinsia unaotekelezwa na Shirika la Kwieco kwa kushirikiana na WFT.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Fuka, Magdalena Magoma, alisema mwanae wa darasa la pili aliiba fedha za mauzo ya mayani Sh.1,000 na kwenda kucheza korokoro na aligundua mchezo huo baada ya tabia ya wizi kushamiri ndani kwake.

Sheria ya Michezo ya Kubahatisha inakataza mtu yeyote aliye chini ya miaka 18 kushiriki ikiwamo kamari au kubeti, inakuwaje watoto wanaachiwa.

Alipotafutwa kuzungumzia madai ya wanaharakati hao kuhusu watoto kucheza korokoro wakati hawaruhusiwi, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Siha, Marko Masue, alisema mamlaka ya kudhibiti vitendo hivyo yanaanzia kwa maofisa watendaji wa vijijiji.

"Nimepokea malalamiko hayo na tutayafanyia kazi, lakini nataka niseme kwamba mamlaka ya kudhibiti kamari hizo iko chini kabisa kule kwa watendaji wa vijijiji. Kama hali iko hivyo muandikieni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Siha ili achukue hatua zaidi," alieleza.

# Mabogini waanza vita dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BARAZA la Maendeleo la Kata ya Mabogini katika Wilaya ya Moshi, limeridhia kuanza kwa kampeni maalum ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa jinsia.

Kata ya Mabogini inaundwa na vijiji nane vya Mtakuja, Mabogini, Mji Mpya, Mvuleni, Mserekia, Chekereni, Muungano na Maendeleo.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na ofisa mtendaji wa kata hiyo Ramadhan Ramadhan, wakati wa semina ya mafunzo kuhusu ukatili yanayotolewa kupitia Mradi wa Paza Sauti kwa wazazi na wanafunzi wa shule za kata hiyo.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kutoa elimu ya jinsi ya kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mradi wa Paza Sauti unatekelezwa na Shirika la kiraia la Tusonge kwa kushirikiana na Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS). Akisoma hotuba ya kuridhia ofisa mtendaji wa Kijiji cha Mtakuja, France Lasway, alitoa rai kwa wazazi na wanafunzi kutumia mbinu walizojifunza kutoa taarifa za vitendo vya ukatili vinavyofanyika katika maeneo wanayoishi.

"Uongozi wa kata umedhamiria kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watu wa jinsia zote pamoja na ukatili kwa watoto ifikapo mwaka 2022. Tunahitaji kushirikiana ili kufikia azma hii", alisema

Kwa upande wake, mjumbe wa kamati ya mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa) katika kata hiyo, John Donald, aliwataka wananchi na taasisi nyingine kuiunga mkono Tusonge katika mapambano yake dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tusonge, Agnatha Zutazaa, iliyosomwa na Mratibu wa Mradi wa Paza Sauti, Joyce Kessy, ilieleza kuwa wanatekeleza mradi huo baada ya maeneo hayo kukabilwa na tatizo la ukatili wa kijinsia.

"Nitoe wito kwa nyinyi mliobahatika kushiriki katika tamasha hili kwenda kutoa elimu kwa wenzenu kuhusu faida na Mtakuwwa ili watoe ushirikiano kwa kamati hizo kufanikisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia na ukatili kwa watoto", alisema Kessy.

Katika tamasha hilo washiriki walipata fursa ya kupata ujumbe mbalimbali uliotolewa na wanafunzi wa Shule za Msingi za Benjamini Mkapa, Fedrick Sumaye na Mserekia.



## Waleta sokoni gari linalogundua na kumaliza kasoro kieletroniki

Ukurasa 19

UCHUMI

# BUFE

Ijumaa Desemba 20, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## MADIWANI WAKUNA VICHWA...

### Waja na Veta mahsusi kwa ajili 'kunusa' fursa za uchumi jirani

Ukurasa 14



# Kampuni za uchimbaji kikaangoni DRC kutumikisha watoto, kuhatarisha maisha

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

Na Sabato Kasika

MADIWANI WAKUNA VICHWA...

# Waja na Veta mahs 'kunusa' fursa za uc



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo (kulia), akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halamshauri hiyo.

KILIMO, ufugaji na uvuvi ni miongoni mwa shughuli za kiuchumi zilizopo katika maeneo mbalimbali nchini, zinazofanywa na asilimia kubwa ya Watanzania, kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Ili kuwepo matokeo mazuri zaidi kiuchumi, jamii inapaswa kuzingatian utaalamu, ambao kimsingi unatokana na uwekezaji wa elimu kwa vijana, inayoendana na fursa za kiuchumi za maeneo husika.

Serikali imekuwa ikishawashauri Watanzania kuachana na mtindo wa kufuga, kulima na kufanya uvuvi wa mazoea, badala yake iwe ya kiitaalam, ili fursa hizo za kiuchumi ziweze kuwanufaisha.

Kimsingi, kilimo, ufugaji na uvuvi ni shughuli za binadamu zinazomsaidia kupata mazao ya chakula na mengine, kwa ajili ya biashara inayomuingizia kipato na kukuza uchumi wake na kujikomboa kiuchumi.

Kwa kutambua umuhimu wa utaalam kwenye sekta hizo, hivi karibuni, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Musoma, lilipitisha hoja ya ujenzi wa vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), kitakachojikita kwenye fursa za kiuchumi za eneo hilo.

**UAMUZI ULIVYO**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma, Charles Magoma anasema, wilaya ya Musoma ina halmashauri mbili na majimbo mawili na chuo kimoja chaVeta, kilichopo Musoma Mjini. Sasa wanataka kujenga kingine Musoma Vijijini, kitakachojikita katika fursa za kiuchumi.

Magoma anasema, baraza hilo liliombwa na mbunge kupitisha uamuzi wa kujenga Veta na kwamba fedha za ujenzi wa chuo hicho atatafuta kwa wafadhili, ili kuhakikisha kinajengwa haraka iwezekanavyo.

"Mbunge wetu Profesa Sospter Muhongo, alitoa ombi hilo muda mrefu na sasa madiwani wamepitisha uamuzi huo, tunaamini ujenzi utafanyika, kwani ndivyo alivyoahidi," anasema Magoma.

Baada ya kufikia uamuzi huo, anasema wamewatuma wataalamu kutoka idara ya ardhi kutafuta eneo la kutosha kwenye moja ya vijiji jimboni humo, ili baadaye taratibu za ujenzi wa chuo hicho zianze.

Anasema, madiwani wameweka mkakati huo wa kujenga chuo cha Veta aina hiyo, ili kuwaisadia vijana ujuzi wa kuwawezesha kutumia na kunufaika na fursa za kiuchumi katika maeneo yao.

"Kwanza kabisa, Musoma Vijijini kuna shule za msingi za serikali ni 111, na za binafsi tatu na shule shikizi ni 10, sekondari za serikali ni 18 na za binafsi mbili, wakati mpya zinazojengwa zikiwa tisa," anasema.

Anasema, wingi wa wahitimu kutoka shule zote hizo unahitaji fursa zaidi za kujiendeleza kwa kupata utaalam unaohusiana na kilimo, ufugaji na uvuvi ili wanapohitimu wafanye shughuli hizo kitaalam kujiletea maendeleo.

**VIJANA NA VETA**

Sitta Peter ni Meneja Uhusiano wa Veta, anayesema bado kuna tatizo kwa vijana nchini linalowabakisha nyuma na wanashindwa kwenda kwenye vyuo vya ufundi kupata ujuzi zaidi, kwa kutotambua fursa za maendeleo kupitia miradi mbalimbali inayowahitaji wenye ujuzi.

"Asilimia 90 ya wanafunzi walioko vyuo vyetu si wazawa wa mikoa ya Shinyanga, Mara na Mwanza, ispokuwa wanaotoka mikoa ambayo haina vyuo, tunaomba jamii iwe na mwamko wa kuwapeleka watoto veta," anatamka Sitta, alipikuwa Kahama.

Meneja huyo anasema, hamasa ya kujiunga na mafunzo Veta ni ndogo, huku fursa nyingi zimekuwa zikichukuliwa na watu kutoka mikoa mbalimbali, ambayo haina vyuo vya ufundi.

"Fursa nyingi, ambazo zinatokana na ujuzi zimekuwa zikichangamkiwa na wageni kutoka nje ya nchi, hali inayowafanya wenyeji wakibaki nyuma wakiilalamikia serikali juu ya ukosefu wa ajira," anasema Peter.

**FURSA VIJIJINI**

Ripoti ya Shirika la Chakula Dunia (FAO-2017) inasema, ili Tanzania na nchi nyingine za Afrika zifikie Malengo Endelevu ya mwaka 2030, ni muhimu zigeukie jamii zinazoishi vijijini kuboresha mfumo wa uzalishaji mazao yao ya kilimo.

FAO inasema, shughuli nyingi za kilimo zinafanywa na wananchi wanaliokoi vijijini, ambao wanaotakiwa kujengewa uwezo wa kiujuzi na teknolojia ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao na kukuza uchumi wa kaya.

Hiyo, inajemnga mtazamo kwamba, iwapo Tanzania itafanikiwa kufanya mapinduzi ya kilimo vijijini, ni wazi itachochea maendeleo ya viwanda na kutengeneza ajira nyingi kwa vijana na hasa wa vijijini.

FAO inasema, licha ya kuwapo kwa mikakati ya kuzikwamua jamii za watu waishio vijijini, kutoka kwenye umaskini, lakini zinakwamishwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu hasa vijana.

Ripoti ya FAO inabashiri kwamba, kati ya mwaka 2015 na 2030, idadi jumuishi ya wakazi wa Afrika na Asia inatarajiwa kuongezeka kutoka bilioni 5.6 hadi zaidi ya bilioni 6.6.

Hivyo, katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, idadi ya vijana walio na umri wa miaka kati ya 15 na 24 inatarajiwa kuongezeka kwa zaidi ya bilioni 90 ifikapo

> **"Asilimia 90 ya wanafunzi walioko vyuo vyetu si wazawa wa mikoa ya Shinyanga, Mara na Mwanza, ispokuwa wanaotoka mikoa ambayo haina vyuo, tunaomba jamii iwe na mwamko wa kuwapeleka watoto veta," anatamka Sitta, alipikuwa Kahama.**

# susi kwa ajili chumi jirani



Mfugaji katika halmashauri inayohitaji Veta.

mwaka 2030 na zaidi ni katika maeneo ya vijijini.

Inaelezwa kuwa, ongezeko la vijana linaweza kutengeneza tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa karne zijazo, kutokana na uzalishaji mdogo kwenye sekta ya kilimo na viwanda.

Katika mazingira hayo, iwapo vijana watapambana kutafuta ajira, matokeo yake ni kwamba wanaokimbia kutoka vijijini kwenda mjini, wataongezeka na kuzidisha umasikini katika maeneo hayo.

FAO inashauri, wanaoishi vijijini waondokane na umaskini, azma ikianzia mna kubaki huko waliko, uamuzi unaopaswa kwenda na mabadiliko ya sera zinazosimamia kilimo na kuongeza uwekezaji wa teknolojia, utakaowawezesha vijana kulima kilimo cha kisasa.



Mkazi wa kijiji cha Murangi, Musoma Vijijini, Simon Kujerwa, akimwagiilia shamba lake la mahindi. Kilimo cha umwagiliaji ni moja ya fursa za kiuchumi katika eneo hilo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Ndivyo ilivyo harusi ya watoto. **PICHA:MTANDAO.**

# Unicef: Ndoa za utotoni balaa na hodi ya umaskini

## *Afrika Kati, Magadacar, Nicaragua balaa

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na masuala ya watoto Unicef, limesema katika ripoti yake mpya kwamba kiasi ya wavulana milioni 115 duniani kote waliingia katika ndoa za mapema.

Ndoa za utotoni ni tatizo linalowakumba wasichana kwa wavulana na kuathiri fursa ya wanandoa hao watoto kupata elimu sahihi na fursa za kazi.

Kuna wavulana milioni 115 duniani kote walio na umri wa kati ya miaka 20 na 24 walioa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 kwa mujibu wa ripoti ya Unicef. Mvulana mmoja kati ya watano kati ya idadi hiyo alikuwa chini ya miaka15.

Utafiti huo wa kwanza, kuangazia ndoa za mapema kwa upande wa wavulana, uliendeshwa katika jumla ya nchi 82 na ulibaini kuwa Jamhuri ya Afrika ya Kati inaongoza kwa ndoa za aina hiyo kwa asilimia 28 ikifuatiwa na Nicaragua asilimia 19 na Madagscar iko nafasi ya tatu na asilimia 13.

Bwana harusi miaka 16 na bibi harusi mwenye miaka 11 baada ya kufunga ndoa India.

Kwenye taarifa yake, Mkurugenzi Mkuu wa Unicef, Henrietta Fore, alisisitiza juu ya athari za ndoa za mapema katika ustawi wa wavulana, na kusema kwamba kitendo hicho kinapora utoto wao.

"Mabwana harusi wavulana wanalazimika kuchukua majukumu ya kiutu uzima ambayo wengi bado wanakuwa hawako tayari.

"Ndoa za mapema zinaleta majukumu ya mapema ya ubaba na kuongeza shinikizo la kuihudumia familia, na hivyo kupunguza fursa za elimu na kazi." Naye mkurugenzi wa chama cha waandishi wa habari Tanzania

Aidha, Unicef inadai kuwa wasichana wameendelea kuolewa katika umri mdogo ambapo binti mmoja kati ya watano katika umri wa kati ya miaka 20 na 24 aliolewa kabla ya kufikisha miaka 18 ukilinganisha na mvulana mmoja kati ya 30.

Ripoti inataja jumla ya watoto milioni 756 duniani kote wavulana kwa wasichana waliingia katika ndoa za umri mdogo na ilibaini watoto wanaoa au kuolewa mapema, wanashindwa kuendelea na shule, hivyo kukosa fursa za kiuchumi na hatari ya kunyanyaswa. **DW**

BIASHARA

# Kampuni za uchimbaji kikaangoni DRC kutumikisha watoto, kuhatarisha maisha

## • Pata mchakato uchimbaji A hadi Z

**Na Mwandishi Wetu**

APPLE, Google, Tesla na Microsoft ni baadhi ya kampuni ziizotajwa katika kesi ya madai ya fidia ya vifo na majeraha ya wachimbaji watoto wa migodi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ni kesi iliyofunguliwa na Mawakili wa Kimataifa wa Haki za Binadamu kwa niaba ya familia 14 za nchini DRC, wakizishutumu kampuni hizo kwa kujua kwamba madini aina ya kobalti yanayotumiwa katika bidhaa zao, yanatokana na ukiukwaji wa sheria kwa kuwaruhusu watoto wadogo kuchimba madini hayo.

DRC inazalisha asilimia 60 ya kobalti inayosambazwa duniani kote. Madini hayo yanatumiwa kutengenezea betri aina ya 'lithium-ion' zinazotumika kuwasha magari ya umeme, kompyuta mpakato na simu janja.

Lakini, hatua za uchimbaji zimekuwa zikizua wasiwasi kuhusu uchimbaji haramu, ukiukwaji wa haki za binadamu na ufisadi.

Kesi hiyo iliyofunguliwa nchini Marekani, madai yao ni kwamba kampuni hizo za teknolojia zilikuwa na "uelewa wa kutosha' kuwa kobalti inayotumika katika bidhaa zao inaweza kuhusishwa na kufanyishwa kazi kwa watoto kinyume cha sheria.

Wanasema kampuni hizo zimeshindwa kudhibiti mifumo ya usambazaji wa bidhaa zao na badala yake, zina faidika kutokana na kuwatumikishwa wa watoto hao.

Kampuni zingine zilizotajwa katika kesi hiyo, ni pamoja na kampuni ya kutengeneza kompyuta mpakato ya Dell na kampuni mbili za uchimba madini za Zheijang Huayou Cobalt na Glencore, ambazo zinamiliki migodi ambayo kwa mujibu wa familia za waathirika, ndiko watoto hao walipokuwa wanafanyia kazi.

Glencore iliiambia gazeti la Telegraph nchini Uingereza kuwa: 'Hainunui, kusindika, wala kufanya biashara yoyote ya madini yaliyochimbwa na wachimbaji wadogo."

Ikafafanua kwanba, haiungi mkono utumikishwaji wowote wa watoto, uwe wa kulazimishwa au hata ule wa kujitolea."

Gazeti la Guardian la Uingereza, limechapisha taarifa ya mifano kadhaa ya wachimbaji watoto waliozikwa wakiwa hai na wengine kuumizwa vibaya baada ya mabomba kuanguka.

Familia hizo 14 zinataka kampuni hizo ziwalipe watoto wao kufanyishwa kazi kwa nguvu, kuumizwa kihisia na kutokuwa na usimamizi makini.

Katika majibu yao, ambayo gazeti la Telegraph, imechapisha, kampuni ya Microsoft inasema kuwa wao wamejikita katika kununua madini ambayo wanafanya uchunguzi wa kutosha wa yanakotokea na kama kuna ukiukwaji wa taratibu na sheria wanachukua hatua.

**DHAHABU INAVYOCHIMBWA**

Ili kupata madini kamili yanayohitajika kwa matumizi, kuna hatua zaidi ya tisa zinapitiwa.

Kazi ya kupasua; Akiwa chini, mchimbaji katika machimbo hutumia kifaa cha kuchimba mawe ya dhahabu kutoka kwenye udongo.

Timu ya uchimbaji huwa na wachimbuaji na wabeba mifuko ya michanga na wachimbaji hutumia saa sita hadi nane chini ardhini kila siku.

Ni kazi inayohitaji nguvu na kwenye machimbo kiasi ya kilo 200 za mchanga hutakiwa kuchimbuliwa ili kupata gramu moja ya dhahabu.

Mifuko ya mawe; Mchimbaji anapitia njia nyembamba, wakati mwenzake akimsubiri. Mifuko ya mawe ambayo husongamana kuelekea upande wa kuingilia machimboni, huwa iko mbele yake.

Machimbo ya dhahabu kama Artisanal huwa ni muhimu zaidi kiuchumi kwa maisha ya binadamu katika eneo la Mashariki mwa DRC.

Kilo 30 kwa mzigo mmoja; Wabeba magunia ya michanga huipeleka kiwandani kwa ajili ya kusafishwa na wanalipwa Faranga za DRC 500, ambayo ni sawa na Euro 0.29, kwa kiwango cha sasa cha kubadilisha fedha Mashariki mwa Kongo kwa gunia moja na wanaweza kutengeneza kiasi cha pesa kwa siku.

Ni miongoni mwa wanaopata kiasi kidogo zaidi cha fedha kwenye machimbo, na katika machimbo haya mara nyingi ni wale walitokea maeneo mengine.

Kufunikwa miamba; Mtu huyu anapiga magoti mbele ya mwamba huku akipasua mawe ya dhahabu kwa kutumia jiwe la kupasulia. Baadaye mawe yanayobaki huvunjwa kwa njia ya kawaida katikati ya miamba ili kupata dhahabu.

Njia hii huchukua muda mrefu, inaweza kuchukua masaa kadhaa kulishughulikia basini moja la plastiki. Wabebaji maji na mawe ya dhahabu huonekana wakipanda na kushuka kwenye machimbo

Udongo wa thamani; Anayemimina udongo wa dhahabu kwenye mtaro wenye kifaa cha kudhibiti kasi. Madini safi huletwa na wataalamu wa kifaa na wanachanganywa na maji na kumwagwa kwenye mtaro wenye udongo.

Kutokana na uzito mkubwa, mawe ya dhahabu yanayosalia huganda kwenye blanketi lililokwa mtaroni, wakati masalia humwagikia chini. Mawe hukusanywa na kuchujwa kwenye beseni la plastiki kwa kutumia mercury.

Mauzo ya awali; Mfanyabiashara kutoka machimbo hayo hukagua kiasi cha dhahabu aliyoletewa. Dhahabu na madini ya mercury yanayoonekana kwenye ndoo ya plastiki ya muuzaji, yakiwa na rangi ya chuma na kijivu kabla ya kusafishwa kiwandani.

Wachimbaji wengi hutarajia kuuza kiwango kidogo cha dhahabu kwa wafanyabiashara wa eneo la machimbo.

Usafishaji dhahabu;Wafanyabiashara wakubwa huunguza dhahabu na tindikali ya Nitric kwenye moto mkali, ili kuondoa masalia yote. Wafanyabiashara hao hushughulika na kiwango kikubwa sana cha dhahabu kuliko wafanyabiashara wa ndani.

Mara nyingi huuza nyingi zaidi kwa wiki. Ziada ya faida yao ni ndogo kuliko wafanyabiashara wa ndani, ingawa huuza kwa kiasi kikubwa na kujihakikishia kipato kikubwa.

Poda thamani & uyeyushaji; Baada ya kuichoma, dhahabu inapimwa kwenye mzani wa umeme. Katika hatua hiyo dhahabu hufikia kati ya asilimia 92 hadi 98 ya uhalisia wake, kwa kutegemea asili yake. Baada ya kuyeyushwa, dhahabu huwekwa kwenye chombo cha kutengenezea umbo. Chombo hicho kikishatolewa kwenye moto mkali wa tanuru, mchimbaji kwenye eneo la kuyeyusha humimina dhahabu iliyoyeyuka kwenye kaboni nyeusi au grafiti kwa ajili ya kutengenezwa umbo.

Ndani ya tanuru, dhahabu hufikia kipimo cha joto la digrii 1,500, Celcius. Huchukua takriban dakika 20 kuyeyusha kilo kadhaa za dhahabu.

Kipindi cha upoozaji; Dhahabu ambayo tayari imeundwa hutolewa kwenye chombo na kuwekwa na wachimbaji kwenye eneo la wazi na wakati huo bado hutoa mvuke wa moto.

Ikiwa na kiwango cha dhahabu cha kilo 4.163 kipisi hiki kina gharama ya takriban dola za Marekani 167,056 kwa bei ya soko la jijini London, Uingereza katika siku iliyozalishwa.


Uzalishaji wa dhahabu kwa mwaka Mashariki mwa DRC unakadiriwa kuwa zaidi ya tani 11, lakini dhahabu nyingi inaendelea kuuzwa bei ya ulanguzi nje ya nchi. Mwaka 2015, wauzaji rasmi wa dhahabu nje ya nchi walirekodi kiasi cha kilo 254.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za mitandao.***



Uchimbaji dhababu.

**"Kilo 30 kwa mzigo mmoja; Wabeba magunia ya michanga huipeleka kiwandani kwa ajili ya kusafishwa na wanalipwa Faranga za DRC 500, ambayo ni sawa na Euro 0.29, kwa kiwango cha sasa cha kubadilisha fedha Mashariki mwa Kongo kwa gunia moja na wanaweza kutengeneza kiasi cha pesa kwa siku.**





Dhahaba iliyokamilika.



Poda ya dhahabu.



Dhahabu udongo wa thamani.



Mchimbaji akitoboa miamba. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# BIASHARA KATIKA PICHA



Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Bugando, Profesa Abel Makubi,(aliyevaa traksuti ya mabaka ya njano) katika maandamano kuelekea uwanja wa CCM Kirumba, kuadhimisha Siku ya Bugando. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**



Mfanyabiashara wa nguo akipanga nguo zake kusubiri wateja katika Mtaa wa Pamba, eneo la Posta jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akitoa Tuzo kwa mwajiri bora wa mwaka 2019, David Magese (kulia), wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), wakati wa hafla ya Tuzo ya mwaajiri bora wa mwaka 2019 iliyoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) Dar es Salaam juzi, kushoto ni Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka na Mwenyekiti wa bodi wa Chama hicho, Jayne Nyimbo.**PICHA: NA MPIGAPICHA WETU**

UCHUMI




Ongezeko la magari, kielelezo cha kuwapo fedha. **PICHA: MTANDAO.**

KIELELEZO

# ‘Pesa zimepotea’ na magari haya kibao yanayoongezeka?

**Na Nimi Mweta**

MOJA ya maeneo yaliyotawala mijadala mitaani sasa, hadi katika baadhi ya majukwaa rasmi ya kiserikali, ni dai la ‘pesa zimepotea mitaani.’ Hapo inatajwa kuwa chanzo baadhi ya biashara ndogo kwa kubwa, kuwa taabani.

Kwa kipindi kilichopita (mwaka 2016 hadi 2017) Benki Kuu ilichukua hatua ya kufunga benki zinazotajwa zilielemewa na madeni. Hatua ya kiserikali, ilikuwa ni kuziunganisha na benki kubwa zaidi.

Viko vielelezo vya fedha kupotea mitaani na kwa jumla ni dhana ambayo hata Rais John Magufuli, huzijibu hoja hizo kwamba “fedha za ujanja ujanja ndiyo zimepotea mitaani.”

**FEDHA HALALI?**

Anasema, vipato halisi vya halali bado zipo bila ya matatizo yoyote. Mtu anaweza kujiuliza, kuwa fedha halali zimeongezeka sana? Hiyo ikiangaliwa upande wa pili wa shilingi, matumizi ya miradi ya maendeleo ambayo kwa jumla yanagusa watu wengi yamepanuka sana. Ni jambo lisilo na mjadala

Mfano hai uko katika Sekta ya Afya, ambayo matumizi yalipanda kufikia zaidi ya mara nane, ikilinganishwa na miaka 2014/2015.

Hiyo inajenga dhana kwamba katika baadhi ya maeneo ambako fedha zimepungua tangu mwaka 2016, utawala uliopo baada ya kuingia madarakani, kuna maeneo kunakoonekana hakuna afueni kwa kipindi chote hicho.

Ni maeneo ambako hakuna sababu za wazi zinazotoa ufafanuzi, ili kupambanua kichwani kwa kutafuta vishikizo vya ishara na mpangilio wa matumizi au upatikanaji wa fedha.

**MAGARI KIELELEZO**

Katika mazingira ya kawaida, mtu anaweza kusema kuwa kununua gari ni kielelezo kimojawapo cha anasa, yaani kuwa na fedha za ziada, kwani wengi tu wananunua kwa mikopo wakiwa na uhakika wa kipato hadi mkopo umalizike.

Ongezeka la magari ya aina hiyo, kiuchumi ni kielelezo cha ongezeko la ajira kwa upande mmoja na ongezeko la kipato kwa upande wa pili. Pia, ni kielelezo sahihi cha ufanisi katika sekta ya fedha na upenyo mikopo.

Kuna wakati, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete katika zama za uongozi wake, alipojadili adha ya foleni, kwamba katika sura ya pili ni kielelezo cha kuboreka maisha ya umma, akimudu kumiliki magari mengi.

Hivi sasa mtu anaweza kujiuliza swali, inakuwaje kuwapo urahisi wa kukopa fedha za kununua magari kwa wingi wakati fedha zimepungua sana mitaani na biashara ziko taabani?

Ni dhana inayofungua njia mbili za kujibu swali hilo. Hiyo inajenga taswira inayohoji usahihi wa swali lenyewe, kwa maana ya kiuchumi

Kuna suala la msingi la kujiuliza, linaloendana na takafakari ya kiuchumi, kama kuna ukweli katika hisia fedha zimepotea mitaani, halafu nusu ya magari yote barabarani sasa hayana zaidi ya miaka mitatu au minne tangu yaandikishwe, inakuwaje?

Nje ya magari, mtu anaweza kuangalia upatikanaji wa pikipiki za abiria. Sasa zimesambaa hadi vijijini na si ajabu hata ni vijiji vyote nchini.

Jinsi barabara za lami zinavyoongezeka katika wilaya na hata baadhi ya vijiji, ndivyo usafiri wa aina hiyo unazidi kuwa ‘bei poa’ na rahisi, kwani haziharibiki upesi.

**MKWAMO UKOJE?**

Kwa kujibu swali la dau la kupotea fedha, kuna majibu ya vielelezo vya kupotea biashara zilizokuwa zinajimudu na kupata wateja kabla ya Januari 2016, baada ya aina fulani ya fedha kuondolewa katika mzunguko.

Mtu anaweza kusema mkwamo huo endelevu ni sehemu ya mashindano, kupotea kwa fedha za ujanja, malipo ya ubabaishaji kwa wafanyakazi na wakala wao, hali inayopunguza matumizi ya kawaida na si anasa peke yake, kama baadhi ya watu wanavyodai.

Ina maana, pia ongezeko la fedha linaloonekana katika ununuzi wa magari halijazi pengo hilo. Ili kupata ufafanuzi wake, kuna njia mbili za kuangalia kutojazwa kwa pengo la mahitaji ya kawaida mitaani, licha ya magari na pikipiki kununuliwa kwa wingi barabarani.

Moja ni mtazamo chanya usioangalia ‘sura ya mtu’ ni kutaka kila biashara ipate wateja, kwa hiyo unatoa tathmini ya masikitiko kuwa kuna ongezeko la tofauti au pengo la mapato kati ya watu, ikidaiwa maendeleo yaliyopatikana tangu mwaka 2016 yamewaacha wengi ‘solemba.’ Ni mtazamo unaoanzia katika haki ya kila biashara kufanana na watu kupata mahitaji yao.

Mtazamo mwingine ni unaoendana na uhalisia wa matumizi ya fedha serikalini, hivyo kupata kielelezo cha kupungua fedha mitaani.

Fedha za ‘ujana’ zilisambaa na kuwafikia wengi, wakiwamo wasiohusika nazo moja kwa moja, kama wapambe.

Athari ikaja zilipofutwa fedha hizo, matumizi ya bajeti (maendeleo bajeti ilikuwa asilimia 26 kabla ya Juni 2016 ikapanda na kufika asilimia 40.

Ni maelezo yanayoendana na kuongezeka magari bila ya fedha kurudi mitaani kwa wingi, kwani ufanisi na ukopeshaji umeendelea kukua kwa wenye ajira au biashara na vipato halisi.

Ni kichekesho na si sahihi uchumi wa nchi kuwa wizi na ubadhirifu serikalini.



> “Ongezeka la magari ya aina hiyo, kiuchumi ni kielelezo cha ongezeko la ajira kwa upande mmoja na ongezeko la kipato kwa upande wa pili. Pia, ni kielelezo sahihi cha ufanisi katika sekta ya fedha na upenyo mikopo.

BIASHARA

# Waleta sokoni gari linalogundua na kumaliza kasoro kieletroniki

## • Wenzao watia shaka ufanisi wake



Maabara ya kisasa ya kukagua magari ya kampuni ya Aurora, jijini Tel Aviv, Israel. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

WAZALISHAJI nchini Israel wametengeneza magari 'yanayojitibu' endapo hitilafu inatokea, likiwa barabarani. Hiyo inafanyika kwa kuwapo mfumo unaowezesha kudodosa mashine na kisha kumaliza tatizo hilo.

Hicho ni Kikundi cha Ujasiriamali na Ubunifu cha Aurora Laboratories (Maabara Alfajiri) cha jijini Tel Aviv, ambako wanasema kuna kifaa muhimu cha kutoa huduma hiyo, kikianza na kukagua gari kwa nje, licha ya kwamba kifaa kimepachikwa ndani ya gari.

Inapotokea kinahisi tatizo, haraka kinashughulikia hitilafu kabla ya gari halijafikia hatua ya kukwama au kusuasua.

Pia, mtambo huo wa ziada unafakinisha ufanyaji kazi wa mitambo ya kuendesha gari na kutoa jumuisho la kinachosababisha kasoro hiyo, bila ya gari kusimama.

Hata hivyo magari hayo hayajaanza kuonekana barabarani, lakini tayari kuna zinazofanana nazo, ambazo zina mitambo ya kidigitali inayofanana na kubadili gari, ikifanya kazi mfano wa kompyuta yenye magurudumu.

**WATAALAMU**

Wataalamu wanasema, mifumo ya kuendesha gari la aina hiyo ni mingi sana, ikikadiriwa inafika milioni 150 ya inavyoingiliana, pia kuoanishwa.

> **"Kihistoria, baadhi ya nchi zimeshaanza kutumia magari yenye maboresho ya kiteknolojia na katika matumizi ya awali, wameshaona adha ya kutegemea mifumo hiyo.**

Nchini Marekani, kipo chombo kilichotua mwezini mwaka 1969 na kuna mifumo 145,000 katika zama hizo kompyuta zilikuwa katika hatua ya kufikirika.

Wanasema magari yanayobuniwa sasa kujiendesha yenyewe yanaweza kuhitaji vijifumo vya aina hiyo bilioni moja.

Gazeti la Israel la Jerusalem Post lilisema kuwa kwa watengenezaji wa magari, wasafiri na gereji au maduka ya vifaa vya magari, kuanza kwa magari yanayotumia teknolojia ya kompyuta au magari ya kidigitali yatazua maswali mengi ya kisaikolojia kwa watumiaji.

Kikubwa bwana siyo yanayoendeshwa kwa mashine za kawaida ambazo hakuna suala la kujitegemea yenyewe, miingiliano imekuwa mingi kiasi cha kushangaza.

Hakuna tena suala la kuangalia injini, matairi na breki kuona kama kuna tatizo, kwani kutakuwa na mlolongo mrefu wa 'vipimo,' yaani viashiria vya digitali kama kuna tatizo linalojengeka jipya.

Ni mapinduzi mapya yanayoingia katika mifumo ya magari na baadhi ya wataalamu wanatia shaka itakuwa rahisi watumiaji kuamini kama mifumo hiyo inafaa na inawalinda kimaslahi.

**WABUNIFU AURORA**

Wabunifu kutoka kampuni ya Aurora Labs, waliofanya mapitio kwa mifumo hiyo ya magari kujitibu, wanaona kuna tatizo, kwani watu wanataka kujua nafasi ya mtu kukaguana kuangalia kama kila kitu kiko sawa, badala ya jukumu kuachiwa digitali kuhakikisha kila kitu kiko salama.

Kihistoria, baadhi ya nchi zimeshaanza kutumia magari yenye maboresho ya kiteknolojia na katika matumizi ya awali, wameshaona adha ya kutegemea mifumo hiyo.

Nchini Marekani, walikoshaanza, kuna jumla ya magari milioni nane yaliyorudishwa kwa watengenezaji mwaka jana, kutokana na ubovu au udhaifu wa mifumo ya kidigitali iliyowekwa.

Kulikuwapo tukio la kuanguka ndege mbili kwa tatizo la kukwama mfumo uitwao 'autopilot' unaotumika katika ndege inayojiendesha yenyewe baada ya kupaa.

Wataalamu wa Aurora Labs wanafananisha mfumo huo na jinsi mwili wa binadamu ulivyo na uwezo wa kugundua tatizo na kulifanyia kazi, bila ya kuwapo msaada kutoka nje, yaani bila daktari au kununua dawa.

Moja ya njia hizo ni kupanda joto mwilini au kuongezeka haraka wa chembe nyeupe (za kupambana na viluwiluwi hasi kwenye damu), licha ya kuwa mara nyingi tu jitihada hiyo ya mwili haitoshi na lazima kuwe na uingiliaji kutoka nje ya mwili.

Wanasema mfumo huo wa gari unajaribu kuiga kile mwili unachofanya, kugundua palipo na tatizo na kulifanyia kazi na kuna teknolojia iitwayo 'line of code behaviour' ikimanaisha, jinsi mtiririko unavyotakiwa kuonekana, gari likiwa linaendeshwa kidigitali.

Hiyo inaelezwa inajengwa katika mfumo wa mashine kujitambua na kuangaliwa na kifaa kilichojengewa ndani ya gari. Ni teknolojia inayowezesha kuelewa kwa kina mifumo ya kidigitali iliyojengewa, katika sehemu zaidi ya 100 zinazodhibiti au kusimamia ufanyaji kazi wa injini na jinsi vinavyohusiana.

Teknolojia inaenda mbali kwa kugusa hitaji la uboreshaji mifumo ya kidigitali inayotumika kwa wakati huohuo inapotokea hitaji au tatizo, bila hata ya tathmini halisi ya awali.

Wataalamu wanasema, teknolojia waliyoiunda inatokana na hitaji la kusahihisha makosa ya mfumo katika kurekebisha uendeshaji mtambo wowote kidigitali, kwani hitilafu inayoangukia eneo hilo ndiyo chanzo cha kurudishwa kwa watengenezaji magari milioni nane nchini Marekani.

Kampuni hiyo, inatajwa kupata dola za Marekani milioni 11.5 za michango kwa ujasiriamali husika tangu iundwe mwaka 2016 na sasa inafuatwa na watengenezaji wakubwa wa magari kutoka Ujerumani, Marekani, Korea na Japan.

Imefungua ofisi maeneo tofauti ikiwamo Michigan nchini Marekani na Macedonia ya Kaskazini (Ugiriki), pia tawi lake karibu na Munich, Ujerumani.

Wanasema kwa hatua, wanunuzi wa magari watataka kujua kiwango cha mifumo ya kugundua matatizo kwenye gari na kuyaondoa bila ya kupoteza muda.

Mwanzilishi wa kampuni hiyo anaamini, teknolojia hiyo itampa mtumiaji uhakika zaidi wa usalama wa gari analotumia, hivyo kupunguza wasiwasi mtu akiwa safarini na familia yake.

Kwa inaelezwa kiufundi, kutumia gari kwa muda mrefu, chanzo cha makosa ya kibinadamu na hata uchovu wa mashine.

UCHUMI

KUTOKA MORO...

# Ilivyokuwa darasa la kinamama kushika usukani wa maendeleo

- M/kiti Halmashauri afunguka miaka 25
- Usemi unaowapotosha sasa 'mguu juu'

**Na Christina Haule, Morogoro**

HAPANA shaka harakati za kuwainua kinamama duniani zimechachamaa. Wana mbinu za kupeana msukumo na kuamshana namna ya kupiga hatua.

Ni mara kadhaa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika nyendo zake za kampeni anawahimiza wajiinue na kujiamini, pia kutobaki nyuma katika masuala yao ya maendeleo.

Upo ushahidi nchini wa maendeleo ya hali ya juu kuwa na safu kubwa ya wabunge na madiwani, mawaziri kinamama, wakiongozwa na Makamu wa Rais, Mama Samia wanachapa kazi katika ulingo wa juu wa usukani unaoliletea taifa maendeleo.

**MORO JE?**

Mjini hapa Morogoro, katika kutafuta kujikomboa kiuchumi na kimaendeleo, kunatolewa wito kwa kinamama kuupuza msemo 'Adui wa Mwanamke ni Mwanamke' na kuimarisha msemo na 'ushindi wa mwanamke unatokana na mwanamke. '

**OFISA MAENDELEO**

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilayani Morogoro, Florence Mwambene, anasema hiyo inasaidia kuua mfumo dume ulioanzishwa unaorudisha nyuma juhudi za wanawake kupiga hatua kwenye kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi, zikiwamo za kisiasa.

Anatoa historia ya msemo 'Adui wa Mwanamke ni Mwanamke, unatokana na historia ndefu ya mfumo dume, ili kumuaminisha mwanamke hawezi kushirikiana kati yao na wakafanikisha lililo la kwao.

Ofisa huyo wa Ustawi wa Jamii, anasema kinamama wengi wana uwezo wa kushirikiana pasipo kuwapo uadui kwenye siasa ya walau kufanya vitu vingi, kama inavyojionyesha kwenye mambo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Florence, wanawake wanapokuwa wengi katika kutimiza jambo, ndio wanajijengea nafasi ya kufaulisha azma zao, zikiwamo katika ulingo wa kisiasa na upigaji kura.

Mama huyo mtaaluma wa maendeleo ya jamii, anahimiza kwamba kinamama wanapaswa kujitokeza kwenye uchaguzi kugombea na wana fursa ya ushindi, kwani wanawake wengi waliopo watamuunga mkono na unakuwa ushahidi wa wazi kuonyesha wanaweza kupeana heshima hiyo.

**M/KITI HALMASHAURI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, anawataka Madiwani wanawake nchini kuzidisha upendo baina yao na kuacha na kujifunza kukaa kimya, ili kuhakikisha wanashika nyadhifa mbalimbali za uongozi kwenye chaguzi mkuu ujao wa viongozi wa kisiasa mwakani. Kingo ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Ngerengere wilayani Morogoro, anaungana kupinga dai "Adui wa Mwanamke ni Mwanamke' akitoa historia yake.

Anasimulia kwamba, katika nafasi zake zote za uongozi, kuanzia



Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, katika maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani, katika zama za uongozi wake mjini, morogoro, mwaka 2015.

> **"Msemo wa Adui wa Mwanamke ni mwanamke usiwagawe wanawake kwenye nafasi za uongozi sababu hauna nguvu yoyote kwa wanawake bali ni msemo wa kisiasa" anafafanua.**

udiwani viti maalum, udiwani wa kuchaguliwa na hadi sasa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, ni wanawake ndio waliomuunga mkono.

Kibena anaendelea kwamba, katika chaguzi zilizopita, mwaka 2010 hadi 2015, aligharamiwa kwa mengi, ikiwemo kuchukuliwa fomu na wanawake wapiga kura wake wa Kata ya Ngerengere.

Anawapa mbinu kinamama wenzake, kwamba suala la kuwa na upendo na kutokuwa na unafiki, linamfanya kiongozi azidi kukua katika nyadhifa zake za uongozi, itakayowasaidia kufikisha idadi sawa ya wanaume na katika uongozi, maarufu '50 kwa 50.'

"Ni namna gani ukiwa kiongozi unavyopaswa kufanya, ikiwemo unapopata nafasi, unaungana nao katika shida na raha na ukiwatenga nao watakutenga" anasema.

Anafafanua Wilaya ya Morogoro ina jumla ya kata 31 za uchaguzi na mpaka sasa kinamama wameshika kata sita tu, akitarajia katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2020, wanawake madiwani kinamama wataendelea kushika nafasi, idadi ya nafasi yao kuanada hata akikaridia walau 10.

Hata hivyo, anakumbusha ni matarajio yasiyokuja kwa kusubiriwa, bali kuidai na kuitafuta na katika kufanikisha hilo. Hivyo, anawataka kinamama wenzake kutokubali kubaguliwa kwa msemo uliopo, ili waweze kufikia lengo wanalokusudia.

Mama huyo anawapa mbinu nyingine wenzake wavunje makundi baada ya uchaguzi na kurudi kuwa wamoja katika maeneo waliopo, iwe jimbo, kata, kijiji au kitongoji, hali inayosaidia kiongozi aliyepo kupiga hatua zaidi bila ya kujali jinsia au atokako.

Anasema, wanawake wanauwezo wa kushika nafasi zilizopo bali iliyotumika ambapo anasema hakuna mtu anayetaka kuachia nafasi kirahisi hasa wanaume, hivyo wameamua kutengeneza hofu kwa wanawake ili kuwawekea ugumu waache kugombea.

"Nilishawahi kuwa diwani viti maalum kwa vipindi vitatu na udiwani wa kata vipindi viwili, yaani nimekuwa kiongozi kama diwani kwa miaka 25. Sasa, wanawake wenzangu msikate tama," anasema Kingo.

**MTAALAMU MWANAZUONI**

Mwezeshaji wa elimu ya Uongozi na Jinsia kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP- Mtandao), Dk. Consolata Sulley, anawashauri kinamama waslhofu misemo inayonula kuwavunja moyo, kwani yaliyopo hata katika familia kwa malengo yake kufaidisha wachache.

Dk. Sulley, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema mara nyingi kuna upotoshaji kwamba wigo wa kisiasa unaaminika kuwa wa mwanaume pekee, jambo ambalo si sahihi na ukweli uliopo, wigo ni wa wote.

Anasema, kuna aina nyingi za kuvunjana moyo kwa misemo, pia kukatishwa tamaa na kunyanyaswa, kudhalilishwa, kutolewa habari au taarifa za kuvunja moyo kupitia vyombo vya habari.

Dk. Sulley anataja mbinu nyingine ya kukatishana tamaa ni kupitia vurugu, hivyo anawaasa wanawake kutovunjika moyo na wasitorudi nyuma, bali wahakikishe wanatimiza malengo waliokusudia binafsi au kikundi.

"Msemo wa Adui wa Mwanamke ni mwanamke usiwagawe wanawake kwenye nafasi za uongozi sababu hauna nguvu yoyote kwa wanawake bali ni msemo wa kisiasa" anafafanua.

Dk. Sulley anaongeza, kwamba haamini dhana hiyo iliyotengenezwa kuwakatisha tamaa kinamama, hivyo hawapaswi kuingia katika mtego wa kimsemo, wakipitia silaha ya kujihami kwa kushirikiana na kufikia malengo yao.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, akiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



# Hospitali binafsi zapewa changamoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI za binafsi zimetakiwa kuongeza ubora wa huduma zake kama kivutio kwa wananchi ili kumudu ushindani unaosababishwa na Serikali kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali nyingi nchini.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa ziara yake kwenye hospitali za binafsi mkoani Mbeya yenye lengo la kujionea huduma zinazotolewa na hospitali hizo kwa wananchi.

Alisema Serikali imefanya kazi kubwa ya kujenga vituo vya afya kila kona nchini hali ambayo inasogeza huduma za afya kwa wananchi ambao awali walikuwa wakipata huduma za matibabu kwenye hospitali za binafsi zilizo jirani na makazi yao.

Alisema ujenzi wa vituo vya afya kila kona nchini unakwenda sambamba na uboreshaji wa huduma za afya kwa kuhakikisha dawa, vifaa tiba na wauguzi wanapatikana kwenye vituo hivyo, na kuwafanya wananchi wasione sababu tena ya kwenda kupata huduma kwenye hospitali za watu binafsi.

Alisema wananchi wanapenda kupata huduma nzuri na za uhakika, hivyo hiyo ni fursa nzuri kwa Hospitali za binafsi kuwekeza kwenye ubora wa huduma ambao utakuwa ni kivutio cha wananchi kwenda kupata huduma kwenye hospitali hizo.

Alisema endapo huduma za afya zitaboreshwa mpaka kwenye hospitali za binafsi, itakuwa ni faraja kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inataka wananchi wake wapate huduma bora bila kujali nani katoa huduma hizo.

Alisema sasa serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imeanza mikakati ya kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanakuwa na bima ya Afya na hivyo kigezo cha wananchi kutokwenda kwenye hospitali za binafsi kwa kuogopa gharama hakitakuwapo na badala yake endapo huduma zinazotolewa huko zitakuwa nzuri wananchi watakwenda kutibiwa kwenye hospitali hizo kwa kutumia bima ya afya.

Akizungumza kwa niaba ya wamiliki wa Hospitali za Binafsi, mmiliki wa Hospitali ya Keys, Dk. Kanama, alisema hatua ya Serikali kuanzisha Bima ya Afya kwa Watanzania imekuwa ni chachu ya Watanzania wengi kupata huduma bora kwenye hospitali yoyote nchini wanayohitaji kutibiwa.

Alisema kwa sasa asilimia 80 ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa kwenye hospitali za binafsi ni wale wenye kadi za bima ya Afya na hivyo kuwapatia wawekezaji wa kwenye sekta ya afya uhakika wa kipato kwenye biashara yao.



Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na maji (Ewura), Titus Kaguo (kulia), akifungua mafunzo ya namna ya kuuza gesi kwa kufuata taratibu kwa wauzaji wa bidhaa hiyo wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, mafunzo ambayo yalitolewa jijini Mbeya. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# NIMRI yafanya utafiti 11 wa kifua kikuu

**Na Mwandishi Wetu,**

TAASISI ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) Mbeya, inaendelea kufanya utafiti 11 wa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) ikiwamo chanjo ili kudhibiti ugonjwa huo kupitia utafiti huo.

Mkurugenzi NIMR Mbeya, Dk. Nyanda Ntinginya, aliwaambia wanahabari wa kampeni ya 'Tumeboresha sekta ya afya' kuangalia mafanikio ya kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019 kituo hicho kimeendelea kufanya tafiti hizo ambapo kati ya hizo nne zinahusu kugundua vimelea vya kifua kikuu kwa kutumia makohozi, damu, mkojo na choo husussan kwa watoto kutokana na changamoto ya vipimo vilivyopo na pia ugumu wa watoto wadogo kutoa makohozi.

Aidha alisema utafiti mwingine unalenga kufupisha matibabu ya kifua kikuu ikiwezekana hadi miezi minne ukilinganisha na miezi sita au zaidi ya sasa.

"Pia utafiti mwingine ni wa chanjo ya kifua kikuu na pia tafiti zingine mbili zenyewe zinalenga kuelewa na kutathmini madhara ya muda mrefu ya kifua kikuu cha mapafu kiafya, kiuchumi na maendeleo mbalimbali," alisema.

Alisema pamoja na shughuli zinazoendelea za kitafiti kituo kimekuwa kikitoa mafunzo ya upimaji na matibabu ya kifua kikuu kwa wahudumu wa afya katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Aidha, alisema kituo kimesaidia kutoa na kutengeneza mashine za GeneXpert katika baadhi ya vituo na hospitali za Mkoa wa Mbeya kama vile kituo cha Afya Ruanda, kituo cha Gereza la Ruanda, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya.

Akizungumzia kuhusu uchunguzi wa sampuli kwa maabara ya NIMR Mbeya, Dk. Ntinginya alisema kituo kina maabara kuu mbili za kutafiti kifua kikuu na magonjwa mengineyo ikiwemo maambukizi ya virusi vya ukimwi(VVU), utambuzi wa mwenendo wa matibabu ya ukimwi, ufanyaji kazi wa ini na figo, minyoo, malaria, kisukari na kemikali kwenye damu.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne NIMR imeongeza ukusanyaji na upimaji wa sampuli za tafiti kutoka sampuli 30, 000 kwa mwaka 2015 hadi kufikia sampuli 40,000 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 25.

"Zaidi ya asilimia 50 za sampuli zilizopimwa zilikuwa ni za damu kwa ajili ya utambuzi wa VVU na magonjwa mengineyo na asilimia 30 zilikuwa za makohozi kwa ajili ya utambuzi wa kifua kikuu,"alisema

Alisema sampuli hizo zilikusanywa kutoka katika kliniki za tafiti za VVU na magonjwa mengine pamoja na kliniki za kifua kikuu zinazoratibiwa na kituo hicho. Alisema NIMR Mbeya ilipatiwa ithibati ya ubora na Shirika la Ithibati za Ubora la Kimataifa la Marekani liitwalo College of American Pathologists (CAP) na kimelinda na kuendeleza ubora huo wa maabara zake kwa kupata cheti cha ithibati kwa miaka minne mfululizo ndani ya awamu hiyo.

"Mwaka 2016 NIMR Mbeya ilifanikiwa kupata fedha kutoka serikali ya Ujerumani takribani Sh. Milioni 150 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maabara ya kifua kikuu ikiwa ni hatua ya kuelekea kuipatia maabara hiyo ithibati ya ubora, na mchakato huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2020,"alisema.

# Serikali yawakumbuka makandarasi wazawa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetangaza kuwa kuanzia sasa itakuwa inawatumia makandarasi wazawa kwenye kazi zote zenye thamani ya chini ya Sh. Milioni 15 kwa lengo la kutoa ajira vijana wa Kitanzania walioopata mafunzo ya Teknolojia stahiki.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Utawala na rasilimali watu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Zaina Mlawa alipomwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kufunga mafunzo ya kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu katika Chuo cha Ujenzi wa Miundombinu ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu kazi (ATTI) kilichopo wilayani Rungwe.

Alisema Wizara itaanza utekelezaji wa utaratibu huo hivi karibuni na hivyo akawataka vijana wanaohitimu mafunzo waunde vikundi ambavyo vitawawezesha kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

"Sheria ya manunuzi inazitaka taasisi za Serikali kutenga angalau asilimia 30 ya fedha za miradi ya barabara kwa ajili ya makundi maalumu ambayo ni ya wanawake na vijana kutekeleza kazi za ukarabati wa miundombinu," alisema Mlawa na kuongeza:

"Sasa ni wakati wenu wahitimu wa mafunzo haya kuchangamkia fursa kwa kuunda vikundi maana hizi fedha hatakiwi kupewa mtu mmoja mmoja na badala yake ni vikundi."

Alisema mbali na serikali kusimamia Sheria hiyo, pia itaendelea kutekeleza sheria zingine ambazo zinataka wazawa wapewe kipaumbele kwenye miradi ya maendeleo.

Mkuu wa Chuo cha ATTI, Mahamoud Chamle, aliiomba Serikali kuwalazimisha wadau wa ujenzi wa barabara nchini kuwatumia vijana wanaopitia mafunzo chuoni hapo ili kuwasaidia kupata ajira.

Aliwataja baadhi ya wadau hao ambao wanatakiwa kulazimishwa kuwa ni Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) ambazo ndio taasisi ambazo zimepewa jukumu la ujenzi wa barabara.

Alisema endapo serikali itafanya hivyo idadi kubwa zaidi ya vijana watajiunga na chuo hicho kupata mafunzo hayo wakiwa na uhakika wa kuajiriwa baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

"Kila mwaka wanahitimu vijana hapa na kwa mwaka huu tupo nao vijana 11 ambao wanahitimu, sasa ili kuwa na uhakika wa chuo chetu kuwa endelevu ni lazima wahitimu wawe na uhakika wa ajira na ajira zao ni shughuli za barabara," alisema Chamle.

Mmoja wa vijana hao, Anitha Gwamaka alisema mafunzo waliyopata yana manufaa makubwa kwao kwa maelezo kuwa yamewapatia ujuzi mkubwa ambao endapo watapewa miradi wataitumia kwenye utekelezaji.



# Waagizwa kushirikiana na wasaidizi wa kisheria

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATENDAJI serikalini wametakiwa kuwapa ushirikiano watoa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yao ili wananchi wanufaike na uwepo wa wasaidizi hao.

Mratibu wa asasi za kiraia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi),Dens Londo, alisema wakati wa ufunguzi wa kongamano la wasaidizi wa kisheria lililoandaliwa na Mtandao wa Msaada wa Kisheria Nchini (LSF) lililofanyika jijini hapa jana .

Londo alisema:"Mpo kisheria na kama kuna watendaji wa serikali wanawakwamisha mnatakiwa kuripoti Ofisi ya Tamisemi ambayo ndio wasimamizi , ikitokea hujapata ushirikiano wasiliana nasi tutamwajibisha mhusika,"alisema

Hata hivyo, aliwataka wasaidizi hao wa kisheria kufuata taratibu na sheria katika utendaji na kuonyesha thamani ya elimu waliyopewa ya msaada wa kisheria ili wananchi wanaonyanyaswa kwa kutokujua haki zao wasaidiwe kuzipata.

Aidha, aliwataka LSF kufuatilia utendaji wa wasaidizi wa msaada wa kisheria ili kuonyesha thamani ya mafunzo na elimu wanayopatiwa.

"Ikiwezekana kuwapima kutokana na utendaji wa kila mtu ili thamani ya fedha inayotumika kuwapa mafunzo ionekane kwenye jamii wanayoishi,"alisema Londo.

Musa Magulu kutoka Wilaya ya Mbalizi anasema wanakabiliwa na changamoto ya uelewa mdogo wa baadhi ya viongozi kutowatambua kwenye maeneo ya utendaji kazi

Magulu alisema kazi yao ya kuelimisha jamii imesaidia kupunguza migogoro midogo midogo iliyokuwa ikijitokeza kwenye jamii na kuimarisha mahusiano bora kati ya watendaji wa serikali katika ngazi ya vitongoji hadi taifa kuhusu maamuzi ya kisheria .

Kwa upande wake ofisa kutoka Mtandao wa Kisheria (LSF), Fortunata Kitokesya , alisema kongamano hilo limeshirikisha wasaidizi wa kisheria zaidi ya 400 kutoka Tanzania Bara.

Alibainisha kuwa LSF kwa kupitia wasaidizi wa msaada wa kisheria wamehudumia kisheria wananchi zaidi ya 27,500 kwa nchi nzima mpaka mwaka huu.

Alisema lengo la kuwafikishia wananchi elimu ya kisheria ni kuondoa migogoro iliyokuwa ikiwasumbua wananchi na hasa akinamama wajane waliokuwa wakinyang'anywa mali walizochuma na wenzao wao kabla ya kufariki dunia.



Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali Kisedet lililopo mkoani Dodoma, Madango Mukama, akizungumza na wadau mbalimbali wakiwamo mahakimu, polisi magereza na maofisa ustawi wa jamii, kwenye semina ya utetezi wa haki ya watoto wanaofanyiwa ukatili iliyofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Wataja mbinu kuokoa watoto mazingira duni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ILI kuondokana na changamoto ya watoto wengi wanaoishi katika mazingira hatarishi hasa mitaani, wadau wametakiwa kuwa na mikakati ya pamoja ya kuwapatia waathirika hao haki zao za msingi ikiwamo elimu, afya ,malazi na chakula.

Mratibu wa Shirika la kuhudumia watoto la Kisedet la Dar es Salaam, Mandogo Mukama, aliyasema hayo jana alipozungumza na wadau wanaoshughulikia haki za watoto waliohusisha mahakimu, polisi, magereza na maofisa ustawi wa jamii kwenye mafunzo yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema ili watoto hao wanaoishi mitaani waondokane na changamoto hiyo wanatakiwa kukaa kwa pamoja na kuwasaidia kutatua kero walizonazo na hatimaye wakanufaika na mpango wa elimu, afya ,ulinzi, malazi na chakula.

Pamoja na wadau kuhusika pia kwa upande wa serikali Wizara ya Afya inatakiwa kuwa na fungu la bajeti itakayosaidia watoto wanaoishi mitaani kujitambua kuwa na wao hawastahili kukaa huko.

Mratibu huyo alisema kwa upande wao shirika hilo limefanya kazi kwa kuwasaidia watoto wa mitaani kuanzia miaka 6 hadi 15 kwa kuwapeleka shule na wa miaka 16 hadi 17 ambao walioacha shule na wapo mitaani kuwaunganisha kwenye vyuo vya ufundi vitakavyowasaidia kupata ujuzi wa maisha yao.

Aidha shirika pia limekuwa likitoa vifaa vya kujifunzia ufundi kama vile vya useremala ushonaji ususi na vya ufundi mwingineo lengo ni kuhakikisha wanapomaliza mafunzo hayo wanajitegemea badala ya kurudi mitaani tena.

Awali akitoa elimu ya mafunzo kwa wadau kwenye semina hiyo iliyoandaliwa na Kisedet mkufunzi wa masuala ya haki za binadamu kutoka chuo cha taaluma ya polisi jijini Dar -es-Salaam, Manyama Wambura, alisema kuwa mafunzo hayo yatawapa uelewa zaidi ya kufanya kazi kwa pamoja.

"Ni matumaini yangu mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ushirikiana wa pamoja ukizingatia kuwa wote hao ni wadau katika kumlinda mtoto katika kupata haki yake dhidi ya ukatili wanaofanyiwa pale inapotokea"alisema

Alisema mafunzo hayo kwa upande wao yatawasaidia kupeana mbinu za ufuatialiaji wa kesi mbalimbali zinazohusiana na ukatili wanaofanyika kwa jamii mbalimbali wakiwemo watu wazima na watoto ambao walio wengi wamekuwa wakikosa haki zao za kimsingi za kisheria.

# Wapigwa msasa kudaka mikopo ya halmashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WADAU wa kutetea maendeleo ya vijana wameanzisha kampeni ya kuwasaidia vijana kupata asilimia 10 ya mikopo inayotolewa katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya maendeleo yao.

Mikopo hiyo hutolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kuwawezesha kuanzisha miradi ya kujitegemea.

Jitihada hizo zinafanywa na taasisi ya Endless Success Foundation kwa kushirikiana na Actioncharge , wanaoshirikiana katika kampeni ya ijue nuru yako ya kesho.

Mkurugenzi wa Endless Success Foundation Amina Feruz, alisema hayo katika warsha ya kiwajengea uwezo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu iliofanyika jijini yenye lengo la kuondoa dhana potofu ya kusubiri ajira serikali badala ya kutumia fursa zilizopo.

Alisema lengo la kuanzisha kampeni hiyo ni kutaka kuwapa muongozo wanafunzi namna ya kupata asilimia 10 ya mikopo inayotolewa na serikali katika makundi ya vijana wanawake na watu wenye ulemavu, ili fedha hizo ziwasaidie kuendesha ujasiriamali.

Vilevile alisema vijana wengi hawajui kama kuna fedha hizo na badala yake wengi wanabweteka mitaani kusubiri ajira serikalini wakati fursa zipo.

Amina aliongeza kuwa taasisi hiyo imeanzisha kampeni ya ijue nuru yako ya kesho ili kuwajengea uwezo vijana pale wanapohitimu vyuo kuacha kubweteka badala yake wafanye kazi ili kusonga mbele.

"Kampeni hii ina lengo la kuwafumbua macho vijana ambao wanalenga kuajiriwa badala ya kutazama fursa zikizopo kujiajiri wao wenyewe,"alisema Amina.

Mkurugenzi wa Action for Charge Organization, Samad Emmanuel alisema imekuwa ndoto yao ya kila siku kuona wanawainua vijana wenzao kuziona fursa na kuzifanyia malengo ambayo yatawawezesha kujikwamua kimaisha.

Alisema taasisi yao imekuwa ikipambana na umaskini hasa kwa vijana wenzao na imekuwa ikijikita katika kutatua changamoto ili kila kijana awe na maisha bora kupitia ujasiriamali.

Mnufaika kutoka Chuo cha Mipango Shamimu Mwanga, alisema kupitia kampeni hiyo amejifunza mambo mengi na kwa hivi sasa ambapo bado wapo vyuoni, baada ya kuhitimu chuo watatumia warsha hiyo iliyobeba ujumbe wa ijue nuru yako ya kesho kujiajiri badala ya kusubiri ajira.

"Warsha hii imetufungulia njia ya nini cha kufanya ili kuweza kumuda maisha yetu endapo ikatokea tumekosa ajira serikalini," alisema Shamimu.

# ACT Wazalendo walia rafu usajili

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha ACT Wazalendo kimeilalamikia Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa kuweka sharti ambalo huenda litakwaza wananchi wanaotaka kujisajili.

ACT Wazalendo inalalamikia uandikishaji wananchi kwenye Daftari la Wapigakura Unguja na Pemba, unaotarajiwa kufanywa mwanzoni mwa mwaka 2020.

Ilisema kigezo kikubwa alichokitaja Mwenyekiti wa ZEC kwa wapiga kura wanaohakiki taarifa zao na wanaoandikishwa upya ni lazima wawe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi ambacho kimehakikiwa na Ofisi ya Usajili wa Matukio Kijamii jambo ambalo ni gumu kwani baadhi ya vijana wamenyimwa fursa hiyo.

Akizungumza na wanahabari Mwenyekiti wa Kamati ya Itikadi, Uenezi na Mawasiliano kwa Umma wa ACT, Salum Bimani, alisema kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi kimekuwa ni sharti la msingi kushiriki katika siasa za nchi kuchagua au kuchaguliwa.

"Hivyo haishangazi kuona ZEC Ofisi ya Msajili wa Matukio ya Kijamii zinafanya kazi kwa karibu katika kufanikisha dhamira ovu ya kuwanyima wananchi vitambulisho ili washindwe kushiriki katika ujenzi wa nchi yao na hasa kuchagua kiongozi na utawala wautakao,"alisema Bimani.

Bimani alieleza kuwa kumekuwa na viashiria na taarifa nyingi za uhakika juu ya yale yanayofanywa na mawakala wa msajili wakiwamo masheha kuwanyima wananchi na hasa vijana barua za kwenda kujisajili katika vituo vya afisi hapo wilayani.

Alisema vijana wengi walionyimwa wamekwamishwa kwa hisia za kisiasa au ubaguzi wa aina nyingine. Bimani alieleza kuwa matendo hayo yanayotokea yamekusudiwa kukijengea mazingira ya ushindi Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi wa mwaka 2020.

"Ndugu wanahabari kwa usiri mkubwa ofisi hiyo ya usajili wa matukio ya kijamii imeanza kutoa vitambulisho vipya kwa wananchi ambao walikwenda kuhakiki taarifa zao na wale wapya ambao hawajawahi kuwa na vitambulisho."

Alisema waamenza kutoa vitambulisho hivyo Jumatatu Desemba 16, 2019 katika Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini kisiwani Pemba.

Alieleza kuwa njama hizo za kupunguza wapiga kura zinazoratibiwa na ofisi hiyo ya matukio ya kijamii zilianzia mbali ikiwamo kutowapatia vitambulisho vijana ambao wamefikia umri wa miaka 18 waliotimiza matakwa ya kisheria ya kuwa na kitambulisho cha ZAN ID.

Wamekwama kwani masheha hawakuwapatia fomu na kuwapunguza wale waliokuwa na vitambulisho kwa hoja ya kuleta uhakiki na kuvifanyia mabadiliko vitambulisho hivyo.

Akijibu malalamiko ya ACT Wazalendo, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Idarous Fauna, alisema ZEC inatarajia kuandikisha wapiga kura 204,752 na kuhakiki 503,580 na kuvitaka vyama vya siasa kuacha kutoa taarifa kienyeji.

Alisema katika uandikishaji huo hakutakuwa na udanganyifu na kila aliyetimiza masharti, mwenye haki na anayekidhi vigezo atasajiliwa na kuhakikiwa na hakuna atakayekwamishwa.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akimkabidhi Cheti cha Shahada ya Uzamili, Muhitimu Khamisuu Hamid Mohamed, katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Tunguu, Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Dk. Shein akipigia chapuo Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Ali Mohamed Shein, amesema wataalamu na wanaotumia Kiswahili wana nafasi ya kuwekeza kwenye njia za kisasa za mawasiliano ili kuchangamkia fursa zilizopo kwenye soko la lugha hiyo.

Alisema fursa hizo ziko upande wa fasihi katika mataifa mbalimbali duniani kwa lengo la kujiongezea kipato.

Akizungumza kwa niaba yake katika kongamano la tatu la Kitaifa la Kiswahili, Makamu wa Pili ya wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, alisema, hadhi ya Kiswahili hivi sasa ni bidhaa muhimu katika kukuza maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni duniani.

Alisema kinachopaswa kuzingatiwa ni jinsi gani itakavyopangwa mikakati ya kuzitumia fursa zinazotokana na Kiswahili duniani.

Alieleza kuwa Serikali ya Zanzibar imekiagiza Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (suza) kifanye maandalizi ya kuanzisha shule ya tafsiri na ukalimali.

Alisema hatua hiyo itawezesha kuandaliwa mapema wataalamu waliobobea wa fani za tafsiri na ukalimali wanaohitajika kwa wingi katika maendeleo mbalimbali ya mawasiliano ikiwemo katika mikutano ya kimataifa ambako Kiswahili kinatambulika hivi sasa.

" Serikali pamoja na kuongeza vifaa na vivutio vyengine maalum vya kuwafanya wageni imeshakiagiza Chuo Kikuu cha Suza kuiimarisha shule ya Kiswahili na Lugha za Kigeni kuwa Kitivo cha kuifanya Zanzibar kuwa 'center of excellence' kituo cha umahiri wa wanaotaka kujifunza lugha washawishike kujiunga," alisema.

Akitoa taarifa ya kongamano hilo Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili Zanzibar, Mwanahija Ali Juma, alisema baraza hilo limekuwa likithamini waandishi wakongwe wa vitabu na kuwaonyesha mwanga wa ukomavu.

Mwanahija, alisema mfumo huo ulioanzishwa na Uongozi wa Baraza la Kiswahili Zanzibar kwa kushirikiana na lile la Tanzania pamoja na taasisi zinazosimamia Kiswahili kimataifa utasaidia kuijengea uwezo na uimara mkubwa lugha ya kimataifa kwa vile tayari imeshaingia ndani ya lugha kubwa duniani.

Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili Zanzibar Dk. Mohamed Seif Khatibu, alisema ushiriki wa viongozi wakuu sambamba na waandamizi wa serikali, taasisi za umma wakiwamo mashirika kiraia kwenye makongamano ya Kiswahili umeonyesha haiba katika muendelezo wa lugha hiyo.

## Wahimizwa kurejesha mikopo kunufaisha wanafunzi wengine

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wahitimu wa Chuo Kikuu cha Tunguu (ZU) waliopata mkopo wa elimu ya juu kurejesha mkopo huo ili unufaishe wengine wengi wanaohitaji fedha za kusoma elimu ya juu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika mahafali ya 17 ya chuo hicho yaliyofanyika huko Tunguu.

Waziri alisema Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania inaufahamu umuhimu wa elimu ya juu ndiyo maana ya kukawekwa kwa mikopo hiyo.

Alisema kuwa wakati umefika sasa kwa wahitimu wa vyuo vikuuu waliopatiwa mikopo kulipa kwa wakati ili kukopesha wengine.

Alisema iwapo wahitimu hawatoweza kulipa mikopo waliopatiwa kwa wakati muafaka, watasababisha wengine kukosa fursa ya mikopo hiyo jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa bodi hiyo.

Alisema kuwapo kwa Chuo Kikuu Zanzibar kumeleta maendeleo ya kiuchumi Zanzibar,Tanzania na Afrika kwa ujumla na kumeongeza wingi wa wanafunzi katika mwaka huu ikilinganishwa na mwaka uliopita ambao ulikuwa na wahitimu 9,344 katika kada tofauti 4,516 wanaume na 4,828 wanawake kutoka serikalini na sekta binafsi.

Mkuu wa Chuo Profesa, Mustapha Adullrahman Roshashi, alisema chuo hicho kinajivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika chuo hicho. Alieleza kuwa hivi sasa chuo hicho kimekuwa na idadi kubwa ya wahitimu kutoka nje ya Tanzania jambo ambalo ni muhimu sana kwa mafanikio ya kitaaluma ya chuo hicho.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Idriss Muslih Hijja, alisema Chuo Kikuu cha Zanzibar ni chuo cha mwanzo kinachoongoza katika kada za masomo mbalimbali na wanatarajia kuongeza miundombinu ya vifaa vya masomo ili kuleta maendeleo kwa wanafunzi waliopo hapo.

Hata hivyo, alisema kuwa mpango uliopo kwa sasa ni kujenga jengo jipya na kuweka ofisi mbalimbali ili kutatua tatizo hilo na kutafuta miradi mbalimbali ya kuongeza kipato kwa wanafunzi na walimu jambo ambalo litasaidia ufanyaji kazi kwa ufanisi mkubwa.

Kwa upande wa wahitimu wa chuo hicho waliiomba serikali kuwapatia ajira ili waweze kulipa mkopo waliopatiwa.

# Singida kutumia mabilioni ujenzi barabara

**Na Elisante John, SINGIDA**

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 10.590 kwa ajili ya miradi mikubwa ya maendeleo mkoani Singida, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ikiwamo ujenzi wa barabara ya Karatu-Mbulu-Haydom-Sibiti-Lalago hadi Maswa (Serengeti bypass) kilomita 389, kwa kiwango cha lami.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Singida, Matari Masige, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji, wa miradi ya barabara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Julai hadi Novemba, mwaka huu.

Akizungumzia mradi wa Serengeti bypass, alisema utekelezaji wake utaanzia barabara ya Mbulu-Haydom (Manyara) yenye urefu wa kilomita 50, huku ikiwa serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 1.45, za kuanza ujenzi huo.

Alisema katika Mkoa wa Singida barabara hiyo inapitia Wilaya ya Mkalama kwenye eneo lenye urefu wa kilomita 78, na itakapokamilika itakuwa kichocheo kikubwa kwa maendeleo ya wananchi wake.

Alibainisha kuwa barabara hiyo inayoanzia Karatu (Arusha)-Mbulu-Haydom (Manyara)-Sibiti (Singida)-Lalago- Maswa (Simiyu), ujenzi wake unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha wa 2019/2020.

Katika hatua nyingine Mhandisi Masige alisema kipindi cha mwaka huu wa fedha serikali imetenga Sh. bilioni 1.45, kuanza kazi ya mradi wa barabara mpya kwa kiwango cha lami, inayotoka Tanga hadi Singida.

Aliitaja barabara hiyo ni Handeni (Tanga)-Kibereshi-Kijingu-Kibaya-Njoro-Olboloti (Manyara)-Chemba-Kwamtoro (Dodoma) hadi Singida, yenye urefu wa kilomita 460, huku katika Mkoa wa Singida ikipita kwenye eneo la urefu wa kilomita 47.1.

"Serikali imetenga Sh. bilioni 4.310, za ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa magari (Osis) kilichopo Muhalala wilayani Manyoni, na Sh. Bilioni 1.5 zingine za ujenzi wa kilomita 25 za barabara ya maingilio kwenye daraja mto Sibiti, kwa kiwango cha lami, lililopo wilaya Mkalama," alisema.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema miradi hiyo yote ikikamilika, husussani ule wa Serengeti bypass, itafungua fursa kiuchumi kwa wananchi wa mikoa inayopitiwa na mradhi huo, kutokana na umuhimu wake kiuchumi.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Biashara ya DCB, James Ngaluko (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi rasmi wa huduma ya mkopo maalumu wa ada ya shule jijini Dar es Salaam jana. Wengine kutoka kushoto ni Balozi wa DCB Skonga, Zamaradi Mketema, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa DCB, Rahma Ngassa na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Fortunata Benedict. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasaidia wilaya mamia masinki ya vyoo

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetoa msaada wa masinki ya vyoo 359 kwa wilaya ya Newala mkoani Mtwara ili yasaidie kuwekwa kwenye baadhi ya vyoo vya shule zinazokabiliwa na tatizo la uhaba wa matundu ya vyoo.

Akikabidhi msaada huo mkoani Mtwara kwa Mkuu wa Wilayani ya Newala, Aziza Mangosongo kwa niaba ya wizara, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, .Dk. Sivia Mauke, alisema katika msaada huo wizara imetoa msaada jumla ya masinki ya sato 2357 kwa Mkoa Mtwara.

Alisema wizara iliahidi kutatua changamoto za uhaba wa matundu ya vyoo katika Mkoa wa Mtwara ikiwa ni kuunga mkono kampeni ya Mkuu wa Mkoa huo, Gelasius Byakanwa ya 'shule ni choo'.

Dk. Mauke alisema katika masinki hayo, 359 yametolewa kwa Wilaya ya Newala ambapo ni miongoni mwa wilaya inayokabiliwa na changamoto ya uhaba wa matundu ya vyoo.

Alisema wizara imeamua kutekeleza ahadi yake kwa vitendo kwa kutoa msaada wa masinki hayo kwa Wilaya ya Newala ili yasaidie kupunguza uhaba huo wa matundu ya vyoo hasa vyoo vya kisasa. Alisema wizara iliamua kutoa ahadi hiyo baada ya kuguswa na kampeni ya 'shule ni choo' inayoendeshwa na Mkuu wa Mkoa na kuona kwa sasa itowe masinki hayo ya sato ili yakutumike kwenye shule zenye changamoto hiyo. Akizungumza baada ya kupokea msaada huo Mkuu wa wilaya ya Newala, DC Mangosongo aliipongeza wizara kwa kutoa msaada huo.

Alisema masinki hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya matundu ya vyoo kwa shule za wilaya hiyo ambazo zinamahitaji makubwa ya matundu ya vyoo.

"Naipongeza sana wizara ya afya kwa kuwa na jicho la tatu la kutuangalia Newala na kutupatia msaada huu ambao utasaidia kupunguza tatizo hili la matundu ya vyoo," alisema Mangosongo

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Byakanwa, aliipongeza wizara ya afya kwa kuendelea kuunga mkono jitihada zake hasa za shule ni choo na sekta ya afya mkoani humo.

## DCB yawakumbuka wenye watoto shule

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI wenye watoto wanaosoma, wamepata fursa baada ya huduma ya kuzinduliwa mkopo maalumu wa ada ya shule.

Uzinduzi huo uliofanywa na benki ya biashara ya DCB ni fursa nyingine itakayowawezesha wateja wa benki hiyo kulipa ada za watoto wao kwa wakati na uhakika.

Mkopo wa ada ni mwendelezo wa mkakati wa benki kubuni huduma na bidhaa bora zinazowanufaisha wateja.

Benki hiyo imekuja na bidhaa hii ya mkopo wa ada katika harakati ya kuwaondolea hofu wazazi linapokuja suala zima la elimu kwa watoto wao sambamba na akaunti ya DCB Skonga inayomuwezesha mtoto kusomeshwa pale mzazi anapopata ulemavu wa kudumu ama kifo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi rasmi wa mkopo huu, Mkuu wa kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa, alisema DCB inaendelea kuleta kwenye soko bidhaa zinazokidhi maisha ya Watanzania.

Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, James Ngaluko aliongeza: ''Mkopo huu ni wa dharura na ni suluhisho kubwa kwa wateja wetu, siku hazilingani na kama benki tunataka watoto wetu wasome, elimu ndio ufunguo wa maisha, hivyo tunampa mzazi fursa ya kupata mkopo wa dharura ndani ya saa 48 kwa ajili ya ada ya mtoto anapokwama.

"Tunaendelea kusherekea sikukuu za mwisho wa mwaka na kukaribisha mwaka 2020, benki tumeona tuwazawadie zawadi ya kipekee kabisa wateja wetu kwani ni jambo lililo dhahiri kuwa suala la ada ni moja ya changamoto kubwa inayowakabili wazazi wengi kila ifikapo mwanzoni mwa mwaka.

Mkopo wa Ada wa DCB una riba ya chini sana na utalipwa moja kwa moja kwenye shule ya mtoto. Mkopo huu unakupa fursa ya kukopa hadi Sh. milioni tano ndani ya masaa 48 na muda wa marejesho unachagua mwenyewe hadi miezi sita."

Mkuu wa kitengo cha Wateja Binafsi, Fortunata Benedict alisema: ''Wazazi wengi kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto wao wamejikuta wakihangaika kutafuta fedha za ada kwa njia zozote, hivyo kujikuta kuingia katika matatizo. Mzazi sasa huna haja ya kupata stress za kulipa ada, acha DCB ikufikirie masuala ya elimu ya mtoto wako hii ni suluhisho la uhakika la kifedha."

## Waandamanaji wapinga marufuku ya polisi

**New Delhi, India**

WAANDAMANAJI mjini New Delhi nchini India, wameapa kuendelea na maandamano wakati polisi ikipiga marufuku mikusanyiko katika mji mkuu na majimbo mengine.

Maandamano kadhaa yamepangwa kufanyika kupinga sheria mpya ya uraia ambayo inawapatia fursa watu wasio Waislamu kutoka mataifa jirani kupatiwa uraia wa India. Sheria hiyo inawagusa Wahindu, Wakristo na wafuasi wa dini nyingine ndogo, ambao wanaishi India kinyume cha sheria lakini wakikabiliwa na mateso katika nchi zilizo na jamii kubwa ya Waislamu za Bangladesh, Pakistan na Afghanistan.

Sheria hiyo iliyopitishwa wiki iliyopita bungeni inafuatia mchakato uliogubikwa na ubishani katika jimbo la Kaskazini Mashariki la Assam ambalo linalenga kuwaondoa watu wote walioingia kinyume na sheria.

Karibu watu milioni 2 katika jimbo hilo waliondolewa kwenye orodha ya uraia na hivyo kutakiwa kuomba upya uraia huo au kuchukuliwa kama wageni.

**DW**

## Bolivia yatoa waranti kumkamata Morales

MWANASHERIA mkuu wa Bolivia, ameamuru kukamatwa kwa rais wa zamani aliyekimbilia uhamishoni Evo Morales, baada ya serikali ya muda kumtuhumu kwa uasi na ugaidi.

Waendesha mashitaka mjini La Paz wametia saini waranti ya polisi ya kukamatwa Morales ambaye kwa sasa anaishi Argentina.

Kiongozi huyo wa zamani aliikimbia Bolivia mwezi uliopita, baada ya ghasia kuzuka kufuatia kuchaguliwa kwake tena katika uchaguzi wa mwezi Oktoba.

Morales aliitawala Bolivia kwa miaka 14 kabla ya kujiuzulu mwezi uliopita na kukimbia.

Awali alipata hifadhi katika nchi ya Mexico na baadae kuwasili Argentina wiki iliyopita.

Waziri wa mambo ya ndani wa serikali ya muda, Arturo Murillo, ametoa mkanda ambao inadaiwa ilirekodiwa ikimuonesha Morales anamueleza mmoja wa wafuasi wake kuzuia magari na kuingilia usambazaji wa chakula katika miji kadhaa.

**DW**

# Hatima ya Trump yabakia mikononi mwa Seneti

JUZI Marekani imeweka historia nyingine baada ya Donald Trump kuingia katika orodha ya rais wa tatu kupigiwa kura ya matumizi mabaya ya madaraka, hatua ambayo atakabiliana na kesi dhidi yake itakayoamua ikiwa atabakia au kuondolewa madarakani.

Bunge la Wawakilishi (Kongresi) lilipiga kura mashtaka mawili ikiwamo rais huyo alitumia vibaya mamlaka yake na kwamba alizuia shughuli za Bunge hilo.

Kura zote zilipigwa kulingana na mitazamo ya vyama, karibu wabunge wote wa chama cha Democtrats walipiga kura kuunga mkono ashtakiwe huku Republican wakipinga kura hiyo.

Wakati kura ilipokua inapigwa, Trump alikuwa akihutubia mkutano wa wafuasi wake.

Trump aliwaambia watu wa Michigan kuwa wabunge hao wamejawa na wivu na chuki kwa kile kinachoendelea nchini humo.

"Wakati tunabuni ajira na kupambana kwa ajili ya Michigan, wenye itikadi kali za mrengo wa kushoto katika Kongresi wamejawa na wivu na chuki na hasira kubwa, unaona kile kinachoendelea." Trump aliwaambia wafuasi wake.

Ikulu ya White House ilitoa taarifa inayosema kuwa rais ana imani kwamba atasafishwa na tuhuma zote kwenye kesi hiyo wakati Bunge la Seneti litakapoitishwa.

Vikao vya Jumatano vya Kongresi vilianza kwa wajumbe wa chama cha Republican kuomba kwanza wapewe utaratibu wenyewe wa siku upigiwe kura wakiwa na nia ya kuvuruga.

Hiyo ilifuatiwa na kura juu ya sheria zitakazotumiwa kwa ajili ya uchunguzi, mchakato uliochukua muda wa saa sita za mjadala wa wabunge wa pande mbili juu ya uhalali, umuhimu na uzito wa mashtaka mawili dhidi ya Trump.

Baada ya majadiliano hayo Bunge la Wawakilishi likaitisha kura kwa ajili ya mashitaka mawili. Shitaka la kwanza likiwa kutumia vibaya mamlaka aliyonayo lililotokana na madai ya kwamba Trump alijaribu kuishinikiza Ukraine kutangaza uchunguzi dhidi ya hasimu wake wa kisiasa Joe Biden, kutoka chama cha Democrats. ,

Shitaka la pili ni kuzuia shughuli za bunge la Kongresi kwasababu rais anadaiwa kukataa kutoa ushirikiano katika uchunguzi dhidi yake, kwa kukataa kutoa nyaraka za ushahidi na kuwazuwia wasaidizi wake kutoa ushahidi katika uchunguzi huo.

Kura katika kipengele cha kwanza cha uchunguzi, cha kutumia vibaya mamlaka zilikuwa 230 ndiyo na hapana 197. Kipengele cha pili cha kuzuwia utendaji wa Kongresi waliokubali 229 na 198 walikataa.

Kuchuguzwa kwa Trump kunamfanya aungane na marais wengine wawili wa taifa hilo walioshtakiwa ambao ni Andrew Johnson na Bill Clinton.

Hata hivyo chama cha Republican kina wawakilishi wengi katika Bunge la Seneti na hivyo anatarajiwa kushinda kesi hiyo na kusalia madarakani.

***BBC***



Raia wa mji wa South Wales huko Australia, akiangalia moto ukiteketeza sehemu kubwa ya mji huo jana **(PICHA: REUTERS)**

# Lebanon yaanza mchakato wa kumpata waziri mkuu

RAIS wa Lebanon, Michel Aoun ameanza mashauriano na bunge kumteua waziri mkuu, ikiwa ni siku moja baada ya waziri mkuu wa zamani Saad Hariri kutangaza kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho.

Mazungumzo hayo awali yalipangwa kuanza siku ya Jumatatu, lakini yalicheleweshwa hadi jana kutokana na ombi la Hariri.

Hariri ambaye ni kiongozi wa kundi kubwa la Waislamu wa Kisuni bungeni, alikataa kutoa maoni alipokutana na rais Aoun jana mjini Beirut.

Lebanon imetumbukia katika maandamano ya nchi nzima tangu mwezi Oktoba yaliyosababisha kujiuzulu kwa Hariri kama waziri mkuu, wiki mbili baadae. Waandamanaji wanataka uongozi mzima kuondoka madarakani wakiwatuhumu kwa utawala mbovu na ufisadi.

Kulingana na katiba ya nchi hiyo, rais anashauriana na bunge kabla ya kumpatia waziri mkuu majukumu ya kuunda serikali mpya

**DW**

# Wahitimu wa vyuo vikuu waonyeshwa ajira samaki

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI na wadau wa maendeleo wameombwa kutoa msukumo mkubwa ili vijana ambao wamemaliza vyuo vya juu na ambao hawana ajira wafuge samaki ili kuinua kipato na kuinua kiwango cha lishe nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari ambao wametembelea shamba la samaki la Wilolesi, katika Kijiji cha Lituta Halmashauri ya Madaba mkoani Ruvuma, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Lucius Luoga, ameiomba serikali kulipa uzito suala ufugaji wa samaki, hasa katika mikoa ya kusini na kusema ufugaji huo una nafasi kubwa ya kuwakomboa kiuchumi na kilishe wananchi wa Wilaya ya Madaba.

"Halmashauri ya Madama ina sifa tosha za kukuza kilimo cha samaki. Tumegundua kwamba kufuga samaki kutainua wananchi kiuchumi, kutaboresha lishe na kilo ya samaki sasa hivi ni Sh. 8,000. Tunashauri mkazo uwekwe kwa vijana waliomaliza vyuo kwa

sababu wamekomaa kuelewa hoja hii. Wanaweza kufanya mawili: ama kufuga samaki wakati wanasubiri ajira wanazotaka au kuufanya ufugaji samaki kuwa ajira yao ya kudumu," aliwaambia wandishi wa habari, na kuongeza kwamba katika mabwawa manne yaliyopo shambani yanalea vifaranga 4,000 wa samaki aina ya sato, na kwamba kila bwawa lina samaki 1,000.

Mkurugenzi huyo alisifu juhudi za sasa za serikali za kuinua kipato cha wananchi vijijini, na kusema serikali ya awamu ya tano imeshajipambanua kuwa ni ya wanyonge na imejipanga kuwaletea Watanzania wote maendeleo.

Kadhalika alisifu kazi inayofanywa na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) katika kubadilisha maisha ya wananchi.

"Maendeleo yanakuja kwa mikakati. Katika ufugaji wa samaki kuna fursa kubwa ya utajiri. Wananchi wa Madaba wakiamua na kusaidiwa kufuga samaki maisha yao kiuchumi yatabadilika. Ufugaji wa samaki ni biashara nzuri ambayo haina hasara," alisema, na kuongeza kwamba vijana wa Lituta wanaanza kuona kwamba kufuga samaki ni kwepesi na kunaweza kutoa ajira. Alisema pia kwamba akiungwa mkono yuko tayari kulitoa shamba litumike kama shamba darasa kwa wananchi wa Madaba.

Kadhalika amesifu kazi inayofanywa na Sagcot katika kubadili maisha ya wananchi.

Alisema ana imani sana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina na anafurahishwa na mkakati wake wa kuinua sekta ya uvuvi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Sagcot, Geoffrey Kirenga, alisema serikali imeanzisha dawati la sekta binafsi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa lengo kuleta mageuzi katika sekta hizo.

"Sagcot ni mdau muhimu katika Dawati hilo. Waziri Luhaga Mpina anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha sekta ya uvuvi inatoa mchango stahiki katika maendeleo ya wananchi," alisema na kuongeza kuwa ufugaji wa samaki unaweza kutoa ajira nyingi kwa wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee (aliyevaa kofia), akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Miungo wilayani humo jana, alipotembelea kuangalia ujenzi wa daraja katikati ya kijiji hicho na Kijiji cha Mbuyuni. MPIGAPICHA WETU

# TPA yaboresha bandari za Uvinza

Na Elizabeth Zaya, KIGOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) inaboresha Bandari za Sibwesa na Lagosa zilizoko wilayani Uvinza mkoani Kigoma ili kurahisisha usafirishaji na kudhibiti bandari bubu.

Akizungumza na waandishi wa habari waliokuwa katika ziara ya Bandari za Ziwa Tanganyika, Meneja wa bandari hizo, Percival Salama, alisema ujenzi wa bandari hizo ni miongoni mwa miradi minne mikubwa inayotekelezwa na mamlaka mkoani Kigoma.

Alisema miradi hiyo iko katika mpango wa mamlaka hiyo kuwa na bandari kubwa katika kila mkoa na wilaya inayopitiwa na maziwa. Akiizungumzia Bandari ya Sibwesa, Salama alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 100, ukihusisha ujenzi wa gati, jengo la abiria, ghala na vyoo.

Alisema kwa sasa meli kubwa inatia nanga katika gati hilo, hivyo kurahisisha usafirishaji wa mizigo mingi pamoja na abiria kwa wakati mmoja.

"Gati la Sibwesa lipo umbali wa saa tatu hadi nne kwa boti kufika nchi jirani ya DRC, mashariki mwa Jimbo la Karemi, hivyo litarahisisha ufanyaji biashara na usafirishaji kati ya Tanzania na DRC," alisema.

Aliyataja mazao yatakayosafirishwa kupitia bandari hiyo kuwa ni pamoja na mpunga, mazao ya uvuvi na mafuta ya mawese ambayo hulimwa kwa wingi mkoani Kigoma. Kuhusu ujenzi wa Bandari ya Lagosa, Salama alisema mradi huo umefikia asilimia 85, ukihusisha ujenzi wa gati, ofisi, jengo la abiria, ghala, vyoo na kibanda cha walinzi.

Meneja wa mradi huo unaotarajia kutumia Sh. bilioni 12.5, Pantaleo Mosha, alisema mradi unaendelea vizuri na kazi kubwa iliyobaki ni kumalizia ujenzi wa gati litakalokuwa na urefu wa mita 180.

Alisema awali eneo hilo halikuwa na bandari rasmi na badala yake wananchi waliegesha boti zao katika sehemu zisizo salama na kufanya biashara bila kuzingatia sheria na usalama wa nchi na hivyo ujenzi wa gati hilo utaondoa matumizi ya bandari bubu.

Alisema bandari hiyo ina uwezo wa kuhudumia eneo la Lagosa na nchi jirani za DRC, Burundi na Zambia, hivyo itafungua fursa kubwa kwa wafanyabiashara wakubwa kusafirisha mizigo yao kwa urahisi zaidi.

# CRB yataka makandarasi kuungana

Na Mary Geofrey

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imewataka makandarasi wazawa nchini kuungana ili kuwa na mitambo ya kisasa na uwezo wa kufanya kazi za miradi mikubwa ya ujenzi inayoendelea nchini.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Consolata Ngimbwa, mudai baada ya kukamilisha ziara ya bodi hiyo ya kukagua miradi mikubwa ya ujenzi wa daraja la Salender, Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na barabara ya njia nne kuanzia Morocco hadi Mwenge.

Alisema katika ziara hiyo wamebaini kuwa, kampuni nyingi za makandarasi wa nje hawashirikishi makandarasi wazawa kwa sababu walizodai ni hawana mitambo ya kisasa ya kutekeleza miradi hiyo na uzoefu wa kutosha.

"Bodi ya CRB tumefanya ziara ya kutembelea miradi mikubwa ya ujenzi katika jiji la Dar es Salaam ili kuona kama kazi zinafanyika kwa usahihi na kusaidia kukuza makandarasi wadogo kwa sababu licha ya kuwa wasajili pia tuna jukumu la kukagua kazi wanazofanya," alisema Ngimbwa.

Alieleza kuwa wanatambua changamoto zinazowakabili makandarasi wazawa na ndio sababu wamekuwa wakiwahimiza kuungana kwa pamoja ili kuunganisha nguvu ili kushirikishwa katika miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali.

Alisema katika miradi waliyotembelea ambayo mingi inatekelezwa na kampuni za nje ya nchi, makandarasi wazawa hawajashirikishwa licha ya sheria kuwaelekeza kufanya hivyo.

Alisema wataendelea kuhimiza utekelezaji wa suala hilo kwa sababu awali walikuwa hawashirikishwi kabisa lakini sasa wanashirikishwa kwa kiasi na mpango uliopo ni kuhakikisha wanashirikishwa kwa asilimia 25.

Naye Mhandisi mzawa katika mradi wa ujenzi wa daraja la Salender, John Shula, alisema ujenzi wa daraja la muda umekamilika na sasa wanaendelea na kazi ya ujenzi wa daraja la Salender linalojengwa ndani ya maji lenye urefu wa Kilometa 1.03.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 / 0784653304 / 0629478005.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


## CHETI KIMEPOTEA



**LUCIA HAMISI KASANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha KIDATO CHA NNE chenye No **S0539/0033** kilichotolewa na NECTA TANZANIA mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/561171/2019.**

115562502

## VYETI VIMEPOTEA



**YVETTE K. ANASEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0530-0082 kilichotolewa na NDWIKA GIRLS SEKONDARI mwaka 2013. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0213-0652 kilichotolewa na MASASI GIRLS SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: 9910811053107.

115561202

## KUPOTEA KWA CHETI



EVANS BASIL EWALA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0189/0026 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia FEZA BOYS HIGH SCHOOL mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
MWB/RB/9165/2019.

115561202

## KUPOTEA KWA KITABU CHA BIMA NA STICKER ZAKE

**ALLIANCE INSURANCE** wanatangaza kupotelewa na Kitabu cha bima na Sticker zake chenye namba **11991251-11991275.**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/OST/RB/554178/2019.

115561402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MAJID HUSSEIN KICHWABUTA.** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota, yenye Namba T 508 ABT, chasis No. TJECB09J613001247, Engine No. 0349622. Kadi ilidondoka na kupotea, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 3/12/2019 na kupewa **No: KAG/BUK/RB/528523/2019.**

Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.

115561102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHIJA MGANGA MACHEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 445 BLA MITSUBISH CANTER. Chassis namba FE317BD442766. Engine namba 4D33865603.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
KBA/RB/8638/2019.

115561002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo PONGWE**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 22/2019**
**Ombi la ENOCH JAMES ABDALLAH kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu FRANCIS ABDALLAH TANDIKO**

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/12/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 19/12/2019
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

115561502


*Uza, Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la**

**Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA**

**YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BUFFON

## AWEKA REKODI YAKE SERIE A




**TURIN, Italia**

KIPA Gianluigi Buffon amefikia rekodi ya Paolo Maldini ya kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati Juventus ikirudi kileleni mwa msimamo baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Sampdoria.

Buffon mwenye umri wa miaka 41, sasa amefikisha mechi 647 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Italia.

Pia amemzidi Alessandro del Piero kama mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa Juve akifikisha mechi 479.

Paulo Dybala na Cristiano Ronaldo kila mmoja alifunga bao moja na kuifanya Juve kukaa kileleni mbele ya Inter Milan kwa tofauti ya pointi tatu.

Dybala alianza kufunga dakika ya 19 na Gianluca Caprari akasawazisha kabla ya Ronaldo kufunga bao la ushindi.

Caprari alitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kuonyeshwa kadi ya njano mara mbili.

Buffon alianza kucheza soka la ushindani akiwa na Parma, ambako alishinda taji la Uefa na Coppa Italia mwaka 1999 kabla ya kuhamia Juventus miaka miwili baadaye.

Akiwa pale Turin, alishida mataji tisa ya Serie A, Coppa Italia mara nne na mara mbili alimaliza nafasi ya pili kwenye Ligi ya Mabigwa Ulaya akiwa chini ya Massimiliano Allegri.

Aliondoka na kwenda kujiunga na Paris St-Germain mwaka 2018, akishida taji la Ligue 1 kwa msimu wake mmoja aliokaa hapo kabla ya kurudi Juventus.

Nahodha huyo wa zamani wa Italia alishida Kombe la Dunia mwaka 2006.

## CITY WAMUWEKEA NGUMU ARTETA

**LONDON, England**

KLABU ya Manchester City bado haijafikia makubaliano ya fidia na Arsenal ambapo inaelezwa ina hitaji kulipwa pauni milioni moja ili kumruhusu Mikel Arteta kwenda kuwa kocha wao mpya.

Arsenal wanamalizia makubaliano ya mkataba na kocha huyo msaidizi wa City mwenye umri wa miaka 37, ili kwenda kuchukua mikoba ya Unai Emery.

Arteta alikuwa Oxford Jumatano kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la Carabao akiwa na City, lakini anatarajiwa kutangazwa kuwa kocha wa Arsenal baadaye wiki hii.

Hata hivyo, City wameweka ngumu kidogo kumuachia kirahisi mchezaji huyo wa zamani wa 'Washika Bunduki' hao.

Inaeleweka kwamba hadi sasa bado makubaliano kamili hayajafikiwa kati ya klabu hizo mbili.

Arteta amekuwa kocha msaidizi wa Manchester City chini ya Pep Guardiola.



## WANAOMHITAJI ZAHA WATANGAZIWA BEI

**LONDON, England**

KLABU za Chelsea, Arsenal na Everton zitalazimika kutoa pauni milioni 80 kupata saini ya nyota wa Crystal Palace, Wilfried Zaha.

Zaha amekuwa akisisitiza anataka kuondoka Palace katika usajili wa dirisha dogo mwezi ujao baada ya kucheza kwa kiwango bora kwa takribani misimu miwili.

Hata hivyo, Palace imetoa masharti kwa klabu inayomtaka inatakiwa kuvunja benki kutoa kiasi hicho cha fedha vinginevyo hatauzwa.

Miamba hiyo mitatu ya England imekuwa ikiwinda saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast bila mafanikio.



Arsenal ilimtengea mshambuliaji huyo pauni milioni 40 katika usajili wa majira ya kiangazi, lakini Palace ilikataa kabla ya 'Washika Bunduki' hao kumsajili Nicolas Pepe akitokea Lille ya Ufaransa.

Zaha, mwenye mkataba unaomalizika mwaka 2023, amekuwa akiwindwa na Chelsea ambayo ipo chini ya kocha Frank Lampard.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 27, amefunga mabao 34 katika mechi 164 alizocheza Palace tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2015 akitokea Cardiff City.

Mwaka 2017 alianza kuitumikia Ivory Coast baada ya kucheza timu ya taifa ya vijana chini ya miaka 19 tangu mwaka 2011.

Zaha amefunga mabao matano katika mechi 17 alizocheza.

## HABARI MICHEZO




# KLOPP:

## MENGI ZAIDI YANAKUJA KWA KEITA

**DOHA, Qatar**

JURGEN Klopp amepaza sauti kuhusu Naby Keita na anaamini kuna mengi yanakuja kutoka kwa kiungo huyo wa Liverpool baada ya kufika fainali ya Klabu Bingwa Dunia.

Keita alianza kuifungia bao Liverpool katika ushindi wa 2-1 kwenye mchezo wa nusu fainali dhidi ya Monterrey juzi Jumatano na kuendeleza rekodi ya kiwango chake bora.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea amefunga mara tatu mfululizo, huku tayari akiwa amefikia mabao aliyofunga msimu uliopita.

Klopp alimsifia Keita na kusema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anaweza kuwa bora zaidi kwenye Ligi Kuu England.

"Naby, ni mchezaji wa aina yake, alifunga bao la maamuzi, alitumia nafasi vizuri," alisema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Hii ndio nguvu, alitumia nafasi vizuri, hivyo imetusaidia sisi. Anakimbia na mpira pale inapohitajika, hiyo ndio tofauti yake.

"Tayari alishafunga bao, na alikuwa na nafasi. Lakini Naby ni mchezaji ambaye anaweza kufunga mabao. Si kwamba ana mechi nyingi alizocheza kwetu sisi, lakini anafunga mabao mengi, na mabao muhimu.

"Kwa uhakika ni mchezaji mwenye uwezo wa kufanya lolote wakati wowote, na kuna mengi zaidi yanakuja. Pengine kama unamjua Naby unaweza kuzungumza mengi zaidi."

## Ronaldo, Dybala sasa wamchanganya Sarri

**TURIN, Italia**

KOCHA w Juventus, Maurizio Sarri amewasifia Paulo Dybala na Cristiano Ronaldo kwa mabao yao dhidi ya Sampdoria, akisema "yalikuwa ya kuvutia."

Dybala alifunga bao la aina yake na Ronaldo akifunga kwa kichwa wakati wakiibuka na ushindi wa 2-1 na kupeleka Juve kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumatano.

Sarri alisifia mabao ya washambuliaji wake hao ambapo alisema walicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi.

"Wakati Ronaldo alipofunga niliona sawa na Dybala kwa hakika walicheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa hakika yalinivutia, wote walifunga mabao ya kufurahishwa zaidi na ushindi ulikuwa ni wa muhimu zaidi."




## Man United inajua jinsi ya kuifunga City - Solskjaer

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesema wachezaji wa Manchester United wanaangalia mbele kuwa na "droo nzuri" baada ya kupangiwa na Manchester City kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la EFL baada ya ushindi wao wa 3-0 dhidi ya Colchester United.

Mabao kutoka kwa Marcus Rashford na Anthony Martial na lile la kujifunga la Ryan Jackson yaliwawezesha 'Mashetani Wekundu' hao kupata ushindi dhidi ya wapizani wao hao kutoka Ligi Daraja la Pili pale kwenye dimba la Old Trafford, lakini Solskjaer anahisi wachezaji wake walikuwa na kiwango bora zaidi.

"Tulitawala mchezo, tulitengeneza nafasi, lakini huwezi kuwa na uhakika hadi bao la kwanza," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa United.

"Walitoka 0-0 dhidi ya Palace na Tottenham, ni wazuri, timu ngumu. Tulitengeneza nafasi za kutosha kipindi cha kwanza na kuwafanya wawe katika wakati mzuri.

"Endapo tukicheza kama vile kipindi cha kwanza na nina furaha kwamba tulicheza vizuri vipindi vyote.

"Tulitengeneza nafasi nyingi kipindi cha kwanza na tulitawala mchezo tulivyotaka."

United itacheza na Man City kwenye nusu fainali mara mbili kati ya Januari 6 na 27, mwakani.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS ALILIA VAR REFA KUIBEBA BARCA

Tuliona wakati wa mapumziko na zote zilikuwa penalti, lakini hatuwezi kulibadili hilo kwa sasa...

**BARCELONA, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, amehoji kwa nini Teknolojia ya Kumsaidia Refa kwa njia ya Video (VAR), haikutumika kutazama faulo mbili za "wazi" alizochezewa Raphael Varane katika eneo la penalti wakati wakitoka sare tasa kwenye mechi yao ya Clasico [dhidi ya Barcelona].

Katika kipindi cha kwanza kwenye Uwanja wa Camp Nou, Varane alishikwa na raia mwenza wa Ufaransa, Clement Lenglet wakati wa pilikapilika kali na kisha alivutwa jezi na Ivan Rakitic wakati akiwania mpira wa kona.

Refa Alejandro Jose Hernandez hakuwazawadia penalti na wala hakuna tukio lolote kati ya hayo mawili lililotazamwa kupitia VAR uwanjani hapo.

Nahodha huyo wa Madrid, Ramos alibaki akiumizwa kwa nini VAR haikuhusishwa, baada ya kutazama matukio hayo wakati wa mapumziko.

"Tuliwaona wakati wa mapumziko na wanaonekana wazi. Na zote zilikuwa penalti, lakini hatuwezi kulibadili hilo sasa," aliiambia Movistar.

"VAR ipo hapa kusaidia. Ilikuwa ni bahati mbaya. Kwa siku nyingine, itakuwa zamu yetu kuwa na penalti ambayo hawatachunguza."

Gareth Bale alifunga bao kipindi cha pili la wazi ambalo lilikataliwa kwa kuelezwa aliotea baada ya VAR kutazamwa, wakati Madrid iliposhindwa kutawala mapema na washambuliaji watatu wa Barca walihaha kurejea mchezoni.

Matokeo hayo yanamaanisha mabingwa hao watetezi, Barca wanabaki kuwa kileleni mwa LaLiga lakini wakiwa pointi sawa na Madrid, ambayo kwa sasa haijapoteza mechi yoyote kati ya 12 ilizocheza kwenye mashindano yote.

Ramos, ambaye katika mchezo huo alikuwa aliweka rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi kwenye historia ya mahasimu hao akiichezea Madrid kwa mara 43, alichanganyikiwa hasa kwa kutambua kibarua kilichopo mbele yao dhidi ya Athletic Bilbao.

"Huwezi kuwa na furaha wakati hushindi, bali kupata kitu fulani hapa mara zote ni chanya," alisema.

"Tumeiona Real Madrid kubwa leo, na utu mwingi, katika uwanja mgumu. Tulienda kuiba mpira, ambao ulitusaidia kutengeneza nafasi nyingi. Kulikuwa na makosa machache na ndiyo matokeo ya mwisho.

"Tulimiliki mchezo vizuri sana. Tulikuwa na nafasi nyingi kuliko wao. Si rahisi kupata mpira mbali nao. Mkakati wa kusukuma mbele zaidi ulifanya kazi vizuri.

"Tunapitia nguvu kubwa katika suala la kucheza na sisi pia ni wazuri kiutimamu wa mwili. Ni aibu mwaka unaisha tungependa hili lisisite.

"Sasa, tunayo Athletic na tunatumai tutaendelea kama hivi baada ya mapumziko."

## KWA UFUPI

**ARTETA KUIGHARIMU ARSENAL**

MANCHESTER City inataka kulipwa pauni milioni moja kutoka Arsenal ili kumwachia kocha msaidizi Mikel Arteta katika mkataba wake, wakati huu 'Gunners' hao wakitaka kumtangaza kiungo huyo wa zamani kuwa kocha wao mpya. ***(Mail)***

**ANCELOTTI, EVERTON WAMALIZANA**

CARLO Ancelotti anajiandaa kutangazwa kuwa kocha wa Everton baada ya kusaini mkataba utakaomuwezesha kulipwa pauni milioni 11.5 kwa mwaka. ***(Mirror)***

**SPURS KUMUUZA ERIKSEN EPL**

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy amesema klabu hiyo haina "hofu" ya kumuuza kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England kwenye dirisha la usajili la Januari. ***(Evening Standard)***

**LIVER YAMGEUKIA MINAMINO**

LIVERPOOL inajiandaa kuachana na mpango wa kumfuata straika wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, 23, katika dirisha la Januari baada ya kukubali dili la kumsajili straika wa Red Bull Salzburg, Mjapan Takumi Minamino, 24. ***(Star)***

**GUARDIOLA AWINDWA PSG**

PARIS St-Germain itajipanga kuipata huduma ya Pep Guardiola na kuihamishia Uwanja wa Parc des Princes kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel. ***(Le 10 Sport via Daily Mail)***

**SANE ATAKA KUTUA BAYERN**

WINGA wa Ujerumani, Leroy Sane, 23, anataka kujiunga na Bayern Munich na anatafakari kuondoka Manchester City dirisha la usajili la Januari. ***(Bild via Mirror)***

**MOURINHO KUJAZWA NOTI**

SPURS itampa kitita cha usajili kocha Jose Mourinho, lakini Mreno huyo hataraji kuingia sokoni Januari, na wakati beki wa West Brom, Nathan Ferguson na mlinzi wa kushoto wa Norwich, Max Aarons, kila mmoja akiwa na miaka 19, wakiwa ni miongoni mwa wanaowawinda. ***(Mail)***

**LIVER, CHELSEA VITANI**

LIVERPOOL, Chelsea na Tottenham ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia mshambuliaji wa Lille, Mnigeria Victor Osimhen, 20. ***(Sky Sports)***

**JUVE KUMBAKISHA DEMIRAL**

JUVENTUS inajiandaa kumbakisha beki Mturuki Merih Demiral, 21, huku kukiwa na tetesi kutakiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England pamoja na AC Milan. ***(Calciomercato)***

**ATLETICO YAMBANIA LLORENTE**

KIUNGO Mhispania Marcos Llorente, 24, anatakiwa na klabu kadhaa Januari lakini Atletico Madrid haitaki kumuuza. ***(AS - in Spanish)***

**LIVER YAMVIZIA GONCALVES**

LIVERPOOL inamfuatilia kwa karibu beki wa kushoto wa Toulouse, Mfaransa Mathieu Goncalves, 18. ***(L'Equipe via Talksport)***

**ARTETA KUANZA NA ZARZANA**

MIKEL Arteta ataanza na kiungo wa Sevilla, Antonio Zarzana, 17, kama usajili wake wa kwanza endapo atateuliwa kuwa kocha mpya wa Arsenal. ***(Estadio Deportivo via Mirror)***

**SSEMEDO AZINGIRWA BARCA**

NYUMBA ya beki wa kulia wa Barcelona, Nelson Semedo ilizilingirwa wakati akijiandaa na mechi ya El Clasico Jumatano. ***(Cadena SER via Marca)***

HABARI MICHEZO

# YANGA NA AZAM, SIMBA VS MTIBWA MAPINDUZI

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MIAMBA ya soka nchini, Simba na Yanga imetenganishwa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyopangwa jana huku ikiangukia kuvaana na Mtibwa Sugar na Azam FC.

Katika ratiba hiyo iliyotolewa jana na waandaaji wa michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Januari 5 hadi 13, mwakani, Yanga imepangwa Kundi A pamoja na mabingwa watetezi Azam FC, Jamhuri ya Pemba na Mlandege ya Unguja.

Wanafainali wa msimu uliopita, Simba wapo Kundi B pamoja na Mtibwa Sugar, Zimamoto na Chipukizi za Zanzibar.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Zanzibar, Omar Hassan Omar 'King', pia imetangaza kamati ya kusimamia mshindano hayo ambayo ni sehemu ya maadhimisho ya Sherehe za Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi ametajwa kuwa ni Sharifa Khamis Salim na Katibu wa Kamati hiyo ni Khamis Abdulla Said. Wajumbe wa Kamati ya michuano hiyo itakayofanyika visiwani Zanzibar, ni Khamis Mussa Omar, Issa Mlingoti, Seif Kombo Pandu, Mohamed Ali Hilali (Tedy), Aiman Othman Duwe, Fatma Hamad Rajab, Salum Ubwa Ali Khalil, Juma Mmanga na Suleiman Pandu Kweleza.

NADAKA...



Kipa wa Simba C, Abdallah Omary, akidaka mpira huku akizongwa na mchezaji wa JKT, Bilal Hussein, wakati wa mchezo wa kirafiki uliopigwa viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Matola: Wachezaji Simba wapo vizuri

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup dhidi ya Arusha United pamoja na michezo ya Ligi Kuu.

Kutokana na mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu Bara yaliyofanywa na Bodi ya Ligi hivi karibuni, Simba itacheza mechi tatu Uwanja wa Uhuru kabla ya Januari 4, mwakani kuvaana na Yanga katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Baada ya kuikaribisha Arusha United kwenye mechi ya Kombe la FA, Desemba 25 itavaana na Lipuli FC huku siku tatu baadaye ikiwa na kibarua kigumu dhidi ya KMC FC kabla ya kufunga mwaka kwa kuikaribisha Ndanda FC hapo Desemba 31, mwaka huu.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola alisema wachezaji wa kikosi hicho wapo vizuri wakati huu wakiendelea na mazoezi na kufafanua kuwa kila kitu kinakwenda sawa.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya Kombe la Shirikisho pamoja na mashindano ya Ligi Kuu," alisema Matola ambaye ataanza kukiongoza kikosi hicho kwa mara ya kwanza msimu huu akiwa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck baada ya Patrick Aussems kutimuliwa.

Naye msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara akizungumzia usajili wa dirisha dogo, alisema kwa upande wao hawana pupa na kudai watasajili kwa matakwa ya kocha wao ambaye anaendelea kukisoma kikosi hicho baada ya kukikabidhiwa hivi karibuni.

Alisema endapo kocha atahitaji kuongeza au kupunguza mchezaji yeyote, watasajili na kudai wapo imara idara zote kwa sasa.

"Sisi hatuna pupa ya usajili tutasajili kwa matakwa ya kocha wetu hatusajili kwa ajili ya kufurahisha watu," alisema Manara.

Aliendelea kusema wanaendelea kujipanga kwa ajili ya kukutana na mahasimu wao Yanga, Januari 4 Mwakani.

# TTCL yawakuna wapenzi wa filamu

**Na Mwandishi Wetu**

WAPENZI wa filamu nchini sasa watanufaika na huduma ya 'T-Burudani' kutoka TTCL itakayomwezesha mteja kupakua, kuhifadhi pamoja na kuangalia filamu aipendayo bila ya kuwa na mtandao wa intaneti.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa kutambulisha huduma hiyo ambayo kwa sasa inatolewa bure, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba alisema kampuni hiyo imeamua kutoa zawadi ya T-Burudani kwa wateja wake hasa wapenzi wa filamu.

"T-Burudani ni huduma itolewayo na TTCL itakayomuwezesha mteja kupakua filamu bila kutumia kifurushi cha intaneti, mteja ataweza kuangalia filamu zote za ndani ya nchi pamoja na kimataifa. Katika huduma hii mteja ataweza kupakua kupitia simu janja ya mkononi pamoja na kompyuta ya kiganjani 'Tablet'," alisema Kindamba.

Akifafanua zaidi Kindamba alisema TTCL katika huduma hiyo imeweka mfumo rahisi utakaomuwezesha, mteja kupakua filamu aitakayo kutokana na maudhui kutoka kote duniani ikiwa ni pamoja na Hollywood, Nollywood, Bollywood, HBO, hata Bongo movies.

Aidha, aliongeza kuwa mteja ataweza kuangalia kwa kipindi atakachohitaji, lakini vile vile ataweza kupakua na kuhifadhi kwa gharama nafuu kupitia 'App'. Sanjari na huduma hiyo alibainisha TTCL imeamua kuwafuata wateja wake maeneo yao kwa kuwatakia heri na sikukuu kupitia kampeni yake ijulikanayo kama 'MTAA KWA MTAA', pia kuwahudumia zaidi.

# WADAU WAITAKA KARETI SHULENI

**Na Friday Simbaya, Iringa**

Wadau wa Kareti wameiomba serikali itambue mchezo huo pamoja na kuweka mitaala yake katika shule za msingi, sekondari na vyuo ili kuweza kuleta nidhamu, kujiamini na kujenga miili kwa vijana.

Aidha, wamesema mchezo huo pia ukitumika vizuri utasaidia kupunguza vitendo vya ukatili na ubakaji kwa watoto wa kike kwa sababu watakuwa na mbinu za kujisaidia pindi wanapokumbana na vitendo hivyo.

Akizungumza mkoani hapa jana wakati mashindano ya kareti, Naibu Meya wa Manispaa ya Iringa, Joseph Lyata Nzalla, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema wameweka bayana mbinu na mikakati ya kuimarisha mchezo huo ili uweze kusaidia kupunguza tatizo unyanyasaji kijinsia katika jamii.

Alisema kuwa mchezo huo ukitumika vizuri unaweza kuwa njia mbadala ya kupunguza viboko mashuleni kwa sababu watoto watajenga nidhamu, unyenyekevu, usikivu na kutotumia hasira kupitia mchezo wa karate.

Mashindano hayo yaliyoandaliwa na Chama cha Karate Mkoa wa Iringa (IKASHOA) na kushirikisha mikoa 12 na klabu zaidi ya 50, yalifanyika kwenye Ukumbi wa CCM Mkoa na kudhaminiwa na Kampuni ya Maziwa ya ASAS, ambapo Mkoa wa Dar es Salaam uliibuka mshindi katika Bonanza la mchezo wa Kareti na kwa ujumla mikoa iliofanya vizuri ni Singida na Iringa.

# Michezo

Ijumaa Desemba 20, 2019

Nipashe




## Ramos alilia VAR refa kuibeba Barca

HABARI UK 30

NO GOAL...!




Gareth Bale akiifungia Real Madrid bao la wazi kabisa kwenye EL Clasico, lakini VAR ikalikataa kwa madai aliotea katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou usiku wa kuamkia jana na kumalizika kwa sare tasa. **HABARI UK. 30**

# USAJILI YANGA KAMA WA DIRISHA KUBWA

## ●●●Yatangaza kumaliza na watano, kishindo kikubwa Jumamosi na Jumanne, huku Niyonzima...

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na juhudi kubwa za Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa kuendelea kuiunganisha, timu hiyo, bado anaweza kukabiliwa na kuanza upya jukumu hilo kutokana na ingizo jipya la wachezaji watano wanaotarajiwa kusajiliwa katika dirisha hili dogo, imeelezwa.

Moja ya matatizo makubwa yaliyoelezwa kuigharimu Yanga kwenye michuano ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Bara wakati huu ikiwa nafasi ya tisa na alama 17 baada ya kushuka dimbani mara nane, ni kukosekana kwa muunganiko wa wachezaji dimbani, tangu ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Mkongomani Mwinyi Zahera aliyetimuliwa.

Yanga ilitolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na kisha kuangukia mechi ya mchujo ya kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo ilitolewa na Pyramids FC ya Misri, hatua iliyosababisha Zahera kutupiwa virago vyake kwa madai ya timu hiyo kucheza ovyo na kukosa muunganiko.

Jambo ambalo wadau wa soka walimtetea Zahera kuwa alihitaji muda zaidi kwa kuwa wachezaji wengi wa kikosi chake walikuwa ni wapya, hivyo alihitaji muda kuiunganisha timu uwanjani.

Hata hivyo, wakati huu dirisha dogo la usajili likiwa wazi hadi hapo Januari 15, mwakani, Yanga ipo sokoni kukisuka kikosi chake upya na tayari imeshanasa wachezaji wawili huku wengine watatu wakitarajiwa kutangazwa kesho, Jumamosi na Jumanne.

Tayari Yanga imekamilisha usajili wa wachezaji wawili, mshambuliaji Tariq Seif aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Misri pamoja na beki wa kushoto kutoka JKT Tanzania, Adeyun Saleh Ahmad, huku Ditram Nchimbi anayeichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC pamoja na kiungo aliyeichezea Simba msimu uliopita, Mnyarwanda Haruna Niyonzima yakiwa ni majina mengine yanayotarajiwa kutangazwa rasmi hadi ifikapo Jumanne.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Klabu Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wanatarajia kusajili jumla ya wachezaji watano na kwamba nyota wengine watatu watatangazwa kuanzia kesho, Jumamosi kabla ya Jumanne kuhitimisha mchakato huo.

"Tumesajili wawili bado watatu kulingana na idara ambazo mwalimu ametaka tuziboreshe, vuteni subra kuna usajili mwingine wa kishindo unakuja Jumamosi na Jumanne tutamaliza. Kuhusu Niyonzima, amesemwa sana lakini subirini tukikamilisha tutawajulisha," alisema.

Hata hivyo, wadau wengi wanaamini kutokana na maingizo hayo matano ambayo wanaeleza ni mapendekezo ya Kaimu Kocha Mkuu, Mkwasa, maana yake ni kwamba ni wachezaji ambao wanatajiwa kuingizwa moja kwa moja kikosi cha kwanza.

"Timu ilipofanya vibaya, Zahera alidai wachezaji wengi ni wapya hawajaelewana jambo ambalo limeendelea kumtesa Mkwasa, sasa wanasajiliwa wapya watano ambao ni chaguo la kocha wa sasa, hii ina maana wataingia kikosi cha kwanza, hivyo kuhitaji muda tena kuzoeana na wenzao wakati huo ligi ikiendelea, sasa nafasi ya kufanya vizuri itatoka wapi?" alihoji Jumanne Almasi wa Mabibo jijini Dar es Salaam.

Naye Cosmas Charles wa Kibaha, Pwani alisema: "Wachezaji watano ni usajili mkubwa sana kwa dirisha dogo, hiyo ni idadi ya kuboresha kikosi katika dirisha kubwa, na kama ni pendekezo kweli la kocha, basi tunaanza kuijenga timu upya, tutarajie timu kumaliza msimu huu vibaya."

# Kili Stars si riziki, Uganda bingwa

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars, jana ilishindwa kupata hata nafasi ya tatu ya michuano ya Kombe la Chalenji kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, baada ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Kenya, huku Uganda ikitwaa kombe hilo nyumbani.

Mabingwa waliopita Kenya ambao walilitwaa kombe hilo mwaka 2017, walifanikiwa kupata ushindi wa pili dhidi ya Kili Stars kwenye michuano hiyo kwa kuifunga mabao 2-1 ikiwa ni baada ya hatua ya makundi kuichapa 1-0. Mabao hayo ya jana yaliyofungwa na Kenneth Muguna dakika ya 15 na Hassan Abdallah dakika ya 35, huku la kufutia machozi la Kili Stars likifungwa kwa mkwaju wa penalti na Gadiel Michael dakika ya 85 baada ya beki mmoja wa Kenya kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari.

Uganda imefanikiwa kulibakisha kombe nyumbani kwa kuichapa Eritrea mabao 3-0, timu iliyoshangaza wengi kwa kufika hatua ya fainali.

Yalikuwa ni mabao ya Anukani Bright dakika ya 32, Kizza Mustapha akifunga bao dakika ya 68, kabla ya Joel Madondo kuhitimisha ushindi kwa kutupia la tatu dakika ya 88.

**Kwa matokeo hayo,Uganda imetwaa kombe hilo ikiwa imeshinda mechi zote sita tangu makundi hadi fainali. Ilianza kwa kuifunga Burundi mabao 2-1, Ikaichapa Somalia 2-0, ikaifunga Eritrea 2-0, kabla ya kuifumua Djibouti 4-1. Kwenye hatua ya nusu fainali ikaichapa Kilimanjaro Stars bao 1-0.**


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >